# Nipashe

Jumamosi Februari 11, 2023 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581218

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US



SUPA JACKPOT
TZS. 1,074,741,067
KWA TZS. 1000 TU!
SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SportPesa.CO.TZ
PIGA *150*87#




**Baba** miaka 30 gerezani kisa kulala na bintiye

UKURASA 3




UKURASA 11

# Kikokotoo mafao bado ni mtihani

UKURASA 2



Rais Samia Suluhu Hassan akimwapisha Rashid Mchatta kuwa Mkuu wa Chama cha Skauti Tanzania, Ikulu Chamwino mkoani Dodoma jana. **PICHA: IKULU**


## Mbaroni tuhuma kuibia marehemu ajali vifo 20 Tanga

• Kiama cha leseni za mchongo chaja... *uk. 3*


REACH A WIDER AUDIENCE THIS
Valentine
SEASON
AT AN AMAZING OFFER
UP TO 25% Off
On valentine season advertisements*
FROM 10th FEB TO 20th FEB 2023
The Guardian
SUPER BRAND LEADING ENGLISH DAILY
Nipashe
YOUR FAVORITE SWAHILI DAILY
TO BOOK YOUR SPACE
PLEASE CALL US TODAY ON
+255 677 020 701
Email: advertise@guardian.co.tz
Or visit us at Mikocheni light industrial area
Opposite ITV / Radio One Dar-es-Salaam
Web: www.ippmedia.com / epaper.ippmedia.com
*Terms and conditions apply.
Followus: @Theguardiantz


## Kifafa; ugonjwa hatari unaotesa zaidi vijana

• Kila watu 1,000 nchini, 37 wanao... *ukurasa. 2*




**MICHEZO** SIMBA YAKAMILISHA HESABU ZA USHINDI UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6



Wanafunzi wakisubiri usafiri katika kituo cha daladala cha Kinyerezi, jijini Dar es Salaam mapema wiki hii. Baadhi ya makondakta wamekuwa wakiwazuia wanafunzi kupanda kwenye daladala kitendo kinachowasababishia kuchelewa shuleni. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Kikokotoo mafao bado ni mtihani

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Waziri Mkuu - Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu kupitia Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa umma (PSSSF) na Mfuko Taifa wa Hifadhi ya Jamii (NSSF), inajipanga kutoa elimu ya kutosha ya ukokotoaji wa mafao kwa watumishi kwa kuwatembelea kwenye maeneo yao ya kazi.

Pia, katika kipindi cha kuanzia mwezi Julai hadi Desemba mwaka jana, waajiri 318 na wanachama 19,656 walihudhuria mafunzo hayo kutoka katika sekta ya umma na binafsi.

Naibu Waziri wa Ofisi hiyo, Patrobas Katambi alibainisha hayo bungeni jana alipojibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Dk. Alice Kaijage aliyehoji kama serikali haioni haja ya kutoa elimu kwa watumishi juu ya ukokotoaji wa mafao.

Akijibu swali hilo, Katambi alisema kazi ya kuwafikia waajiri na wanachama wengine ili kuwapa elimu husika inaendelea.

"Serikali inaendelea kusimamia na kuratibu na kuhakikisha elimu ya umma inatolewa kupitia makundi mbalimbali yanapokuwa na vikao kama mabaraza ya wafanyakazi, semina, warsha, makongamano, pia mfuko unaendelea kuwatembelea watumishi kwenye maeneo yao ya kazi na kuandaa na kuwashirikisha katika vipindi kwenye runinga na mabango kwenye mitandao ya kijamii," alisema. Katika swali la nyongeza, mbunge huyo alihoji katika fomula ya kikokotoo kilichopita, watumishi wengi walishakopa na wanaostaafu kwa sasa walishakopa, hivyo akataka kujua kama serikali ilishaliona hilo na hatma yao ni nini.

"Kikokotoo cha sasa kimekuja na fomula nyingine ambayo wanatoka na mafao yao ni zaidi ya nusu hawajapata. Je, serikali ni nini hatma ya watumishi hawa ambao mafao yao yalishaivа na walishakopa kupitia fomula iliyopita?" alihoji.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Katambi alisema" "Kabla ya kufanya uamuzi huo, mchakato ulishirikisha wadau wote na kuliandaliwa 'actuarial report' na tulibaini mambo ambayo mbunge aliyasema na kikokotoo kipya kimeongeza pato la kila mwezi tofauti na kikokotoo cha awali ambacho hakikuleta tija zaidi."

Sakata la kikokotoo cha mafao ya wastaafu liliibuliwa na gazeti hili mwaka 2018 baada ya kuripoti kwa kina kuhusu kanuni ya sheria iliyoanzisha mfuko wa PSSSF baada ya kuunganisha mifuko ya PPF, PSPF, LAPF na GEPF, uamuzi ambao pia uliwezesha nchi kuwa na mifuko miwili ya PSSSF na NSSF.

Kutokana na habari zilizoandikwa mfululizo, aliyekuwa Rais kipindi hicho, Hayati Dk. John Magufuli, aliagiza kusitishwa kutumika kwa kanuni za sheria hiyo hadi mwaka 2023, lakini kabla ya kufikia wakati huo serikali kwa kushirikiana na wawakilishi wa wafanyakazi walifikia uamuzi wa kuwa na kikokotoo kimoja cha asilimia 33. Kikokotoo kilichokuwa kimependekezwa awali kwenye kanuni za sheria mpya ya NSSF ambao ni mfuko wa sekta binafsi, ni kuwa mkupuo wa asilimia 25 na mifuko mingine ya watumishi wa umma asilimia 50, sasa watumishi wote wanapostaafu wanapata mkupuo unaofanana wa asilimia 33.

# Kifafa; ugonjwa hatari unaotesa zaidi vijana

## -Asilimia 10 tu ya wagonjwa wanafika hospitalini
## -Wengi hukimbilia kwa waganga wa jadi, manabii

**Na Mary Geofrey**

WAKATI takwimu zikionyesha idadi ya waathirika wakubwa wa ugonjwa wa kifafa ni vijana, wanaofika hospitalini kupata matibabu ni asilimia 10 pekee.

Pia imebainishwa kuwa asilimia 36 wanaamini ugonjwa huo unatokana na ushirikina, asilimia 75 wanakimbilia kwa waganga wa jadi na wengine nyumba za ibada.

Hayo yalibainishwa jana na Mjumbe wa Chama cha Wataalamu wa Ugonjwa wa Kifafa nchini (TEA), Dk. Patience Njenje alipozungumza na waandishi wa habari kuelekea Siku ya Kifafa Duniani itakayofanyika Februari 13 mwaka huu ikiwa na kaulimbiu ya 'Tokomeza Unyanyapaa'.

Alisema duniani watu milioni 60 wanaugua ugonjwa huo, kukiwa na ongezeko la wastani wa wagonjwa 200,000 kila mwaka na nchini ni wagonjwa 37 katika kila watu 1,000.

Alisema sababu ya vijana wenye umri wa wastani wa miaka 15 kuongoza kuugua ugonjwa huo, ni rika ambalo wengi wanapata ajali zikiwamo za bodaboda na kupata uvimbe kichwani.

"Unaweza ukapata ajali ukaumia kwenye ubongo usijue, baada ya miaka mitatu hadi mitano ukaanza kuanguka kifafa.

"Kwa watoto wanapata tatizo hili mama anapopata uchungu pingamizi wakati wa kujifungua, mtoto anapozaliwa halii, baadaye akiwa mkubwa, anaanza kudondoka kifafa, ndio sababu ya vijana wengi kuwa na tatizo hili," alifafanua.

Dk. Njenje alisema asilimia 25 ya wagonjwa wa kifafa wana ulemavu unaotokana na majeraha wanayopata pindi wanapoanguka.

"Wengi wetu hatujui namna ya kumpa huduma ya kwanza mgonjwa mwenye kifafa, usimkamate viungo vyake anapoanguka kwa sababu kinachotingishika ni ubongo, ukimbana unaweza kumvunja viungo," alisema Dk. Njenje.

Alionya pia mgonjwa anayepata kifafa hatakiwi kuwekwa kijiko wala kijiti mdomoni ili kuzuia asijing'ate ulimi kwa sababu anaweza kurudisha ulimi ndani akabana pumzi na kusababisha kifo.

Alionya pia matumizi ya nyama za nguruwe ambazo hazijaiva vizuri kwa sababu zina minyoo inayosababisha ugonjwa huo.

Dk. Njenje pia alisema asilimia 45 ya watoto wenye tatizo hilo, hawapelekwi shuleni na asilimia 68 mahudhurio yao hayaridhishi na asilimia 37 ndio wanapata elimu ya msingi.

"Watoto hawa hawaruhusiwi kucheza na wengine, hufichwa katika jamii na baada ya mgonjwa kuathirika kwa asilimia tano hadi 10 ndipo hupelekwa hospitalini kupata matibabu.

"Ifahamike kuwa mwenye tatizo akichelewa matibabu yake pia huwa yanakuwa juu zaidi," alisema Njenje.

**AINA ZA KIFAFA**

Mtaalamu huyo wa Mishipa ya Fahamu, Ubongo na Uti wa Mgongo anataja aina mbili za kifafa kuwa ni cha kuanguka na kupoteza fahamu (kikubwa) na msuli au kiungo kimoja cha mwili kutikisika (kidogo).

Dk. Njenje alishauri katika kudhibiti tatizo hilo, mama mjamzito ahudhurie kliniki wakati wote wa ujauzito, kutibu watoto wanaopata ugonjwa wa homa, matumizi ya vyandarua, choo bora na kula nyama za nguruwe zilizoiva vizuri.

Alisema katika kuadhimisha siku hiyo, wanaiomba serikali kutoa dawa za kutosha kwa wagonjwa kwa kuwa gharama za matibabu ni kubwa na wengi hawamudu.



Baadhi ya wanachama wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), wakichimba msingi, kwa ajili ya kujenga ofisi ya chama ya wilaya, eneo la Nyakato, mjini Musoma, mkoani Mara jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mbaroni tuhuma kuibia marehemu ajali iliyowaua ndugu 16 Tanga

**Na Waandishi Wetu**

JESHI la Polisi Mkoa wa Tanga linawashikilia watu 14 wakituhumiwa kuhusika na vitendo vya kuwaibia marehemu wa ajali ya basi dogo la abiria na lori wilayani Korogwe wiki iliyopita.

Ajali hiyo ilitokea usiku wa Februari 3 mwaka huu, ikisababisha vifo vya watu 20 wakiwamo ndugu 16 waliokuwa wakisafirisha mwili wa Athanas Mrema kutoka Dar es Salaam kwenda Rombo kwa ajili ya maziko.

Hatua hiyo inatokana na malalamiko kwamba watu waliwaibia marehemu wa ajali hiyo, Jeshi la Polisi likifanyia kazi taarifa hizo na kubainisha kuwa watu hao wanahojiwa ili kujua ukweli wa madai hayo.

Kamanda wa Polisi mkoani Tanga, Henry Mwaibambe aliwaambia waandishi wa habari jana kuwa watu hao wanahojiwa kutokana na kutuhumiwa kuhusika na vitendo hivyo.

Kamanda Mwaibambe alisema wanashirikiana na ndugu wa marehemu maana wao ndio wa kwanza kufika eneo la tukio la ajali hiyo kutokana kwa kuwa walikuwa wanafuatana kwenye magari wakati wanasafirisha mwili huo.

"Walikuwa na Coaster mbili zilizokuwa zimefuatana na walifika Korogwe saa mbili na nusu usiku, wakapata chakula na kupitia sheli kwenda kuweka mafuta na Coaster ya pili ndio wa kwanza kushuhudia hiyo ajali," alisema.

Kamanda Mwaibambe alisema dereva wa Coaster alibanwa mguu na alipata nafasi ya kumwita ndugu yake na kumpatia simu.

Hata hivyo, alisema kuwa jana ndugu walimaliza matanga na baadaye watajua vitu gani viliibwa huku akieleza kwamba hivi sasa wao wanaendelea na uchunguzi.

**LESENI MCHONGO**

Wakati hayo yakiendelea mkoani Tanga, serikali imesema kuwa kutokana na wimbi la ajali za barabarani katika siku za hivi karibuni, imeanza kuchukua hatua ikiwamo kufanya uhakiki wa mifumo ya utoaji leseni ndani ya Jeshi la Polisi na taasisi nyingine.

Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Hamad Yusuf Masauni alibainisha hayo jana jijini Dodoma alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu matukio ya ajali hizo zinazogharimu maisha ya watu na kusababisha majeraha.

Masauni aliyezitaja ajali za hivi karibuni Tanga na ya juzi mkoani Dodoma iliyosababisha vifo vya watu 12, alisema: "Tumenza kuchukua hatua na hatua ya kwanza ni kufanya uchunguzi lakini uchunguzi wa awali unaonyesha kuwa ajali hizi zinatokana na makosa ya kibinadamu, unaweza kusema ni uzembe wa madereva.

"Serikali inapanga kuanza operesheni ya kufanya ukaguzi wa shule zote za udereva, kukagua dawati la utoaji leseni la ndani ya Jeshi la Polisi pamoja na mfumo wa utoaji leseni wa Mamlaka ya Mapato (TRA).

"Tunakwenda kufanya ukaguzi kwenye shule zote za udereva nchini ili kuona ni jinsi gani wanatoa mafunzo ya udereva na kwenye shule hizo kuna uadilifu kiasi gani pia weledi unazingatiwa kwa kiasi gani, pia tunakwenda kukagua dawati la utoaji leseni la Jeshi la Polisi kuona namna ambavyo leseni zimekuwa zikitolewa kama zinazingatia sifa, taratibu na sheria za usalama barabrani.

"Pia tunakwenda kuhakiki mfumo wa utoaji wa leseni TRA kama madaraja ya leseni yanayotolea ni yale ambayo yameidhinishwa na Jeshi la Polisi na siyo vinginevyo".

Waziri huyo pia alisema wanakwenda kufanya uhakiki wa madereva wa mabasi na malori nchi nzima ili kuwasajili kwenye mfumo kupitia Mamlaka ya Udhibiti Usafiri wa Nchi Kavu (LATRA) na ambaye hatatimiza vigezo, hataruhusiwa kuendesha chombo cha moto.

"Hatuwezi kuendelea kuvumilia uzembe huu kwani hata ajali ya juzi iliyotokea Kongwa uchunguzi unaonyesha waliendesha basi lile walikuwa siyo madereva, madereva wenyewe wamekutwa ni majeruhi wodini," alisema.

Mkuu wa Jeshi la Polisi nchini, IGP Camillus Wambura alisema wanakwenda kuhakiki mawakala wa utojai leseni na ambaye atabainika kukiuka utaratibu, hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi yake.

IGP Wambura pia alitoa wito kwa wananchi kushirikiana na Jeshi la Polisi kutoa taarifa za vitendo vya rushwa kwa baadhi ya askari polisi ambao wamekuwa wakilichafua jeshi hilo pamoja na serikali kwa ujumla.

***Imeandaliwa na Paul Mabeja (DODOMA) na Oscar Assenga (TANGA).**

# Baba jela miaka 30 kwa kulala na binti yake

**Na Neema Hussein,** MPANDA

MAHAKAMA ya Wilaya Mpanda, imemhukumu Agustino Michese (59) kutumikia kifungo cha miaka 30 jela baada ya kupatikana na hatia ya kufanya mapenzi na mtoto wake wa kumzaa mwenye umri wa miaka 16.

Hukumu hiyo ilitolewa jana na Hakimu Mkazi Mwandamizi Rebecca Mwalusako, kutokana na mshtakiwa kufanya kosa hilo kinyume cha kifungu cha 158, kifungu kidogo cha (1) (a) cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu Sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marejeo mwaka 2019.

Alisema mshtakiwa alitenda kosa hilo tarehe tofauti kati ya Mei hadi Desemba, 2022 katika kijiji cha Isinde, Mpanda mkoani Katavi.

Pamoja na kutiwa hatiani, mshtakiwa wakati akisomewa maelekezo ya awali, alikiri kutenda kosa hilo huku akijitetea alikuwa amelewa, hivyo alijua anayefanya naye tendo hilo ni mke wake.

Katika kujenga kesi hiyo, upande wa mashitaka ulipeleka mashahidi watano akiwamo mtoto aliyefanyiwa kitendo hicho (jina linahifadhiwa). Wakati akitoa ushahidi, alidai kuwa baba alimfanyia kitendo hicho mara tatu huku akimtaka kutopiga kelele na kama angefanya hivyo, angempiga na kumfanyia kitu kibaya.

Pamoja na vitisho hivyo, alidai kuwa alichukua uamuzi wa kumweleza shangazi yake kutokana na kile anachofanyiwa na baba yake huku akidai hakumwambia mama yake kwa sababu ana matatizo ya akili, hivyo alihofia akimwambia hatalifanyia kazi suala hilo.

Shahidi mwingine ambae ni daktari aliyemfanyia vipimo mtoto huyo, aliiambia mahakama kuwa uchunguzi wa kitabibu ulibaini kuwa mtoto huyo aliingiliwa.

Alidai kuwa mbali na kubainika kuingiliwa, pia mtoto huyo ilibainika kuwa ameambukizwa magonjwa ya zinaa na kwamba baba yake baada ya kufanyiwa vipimo, aligundulika kuwa na maradhi hayo.

# Miili yatambuliwa ajali ya basi iliyoua watu 12

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MIILI tisa kati ya 11 iliyofikishwa kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro kutokana na ajali ya basi la Kampuni ya Frester usiku wa kuamkia juzi wilayani Kongwa mkoani Dodoma, imetambuliwa huku vilio na simanzi vikitawala nje ya chumba cha kuhifadhi maiti.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali hiyo, Dkt. Kessy Ngarawa alisema jana kuwa miili tisa kati ya 11 tayari imetambuliwa na kuchukuliwa na ndugu zao.

Alisema miili iliyobaki ni pamoja na wa mtoto wa kike mwenye umri wa kati ya miaka minne na mitano na mwanamume.

Wakizungumza na Nipashe nje ya chumba cha kuhifadhi maiti cha hospitali hiyo, baadhi ya ndugu wa marehemu walieleza kusikitishwa na ajali hiyo na kuiomba serikali kuchukua hatua madhubuti kwa madereva wanaokiuka sheria na kanuni za usalama barabarani.

Miili hiyo 11 iliyopokewa Morogoro ni kati ya 12 waliopoteza maisha kwenye ajali iliyotokea majira ya saa tisa usiku wa kuamkia juzi kwenye Kijiji cha Silwa, Kata ya Pandambili wilayani Kongwa. Majeruhi wa ajali hiyo wanakadiriwa kufikia 63.

**MAJERUHI DODOMA**

Kwenye Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma, majeruhi wanane wamebaki wakiendelea kupatiwa huduma hospitalini huko baada ya wenzao kuruhusiwa kuondoka. Ajali hiyo ilihusisha basi la abiria mali ya kampuni ya Frester yenye namba za usajili T 415 DPP lililokuwa linatoka Bukoba kwenda jijini Dar es Salaam na lori aina ya Texas likitoka Dar es Salaam kwenda Dodoma.




Mwenyekiti wa Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), Deodatus Balile (katikati), akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akiishukuru serikali kwa kusoma muswada wa marekebisho ya Sheria ya Huduma ya Habari 2016 Bungeni. Wengine ni wajumbe wa Kamati ya Utendaji ya Jukwaa hilo, Angel Akilimali (kulia) na Salim Said Salim. **PICHA: IMANI NATHANIEL**

# Muswada kuifumua Sheria ya Habari wawasilishwa bungeni

**Na Romana Mallya**

HATIMAYE mchakato wa kuifanyia marekebisho Sheria ya Huduma za Habari, 2016 ulioibua mvutano kati ya Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari na Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF), umetulizwa baada ya jana serikali kuwasilisha bungeni Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria mbalimbali, ikiwamo sheria hiyo.

Mbali na muswada huo, serikali pia imewasilisha Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi kwa lengo la kuondoa upungufu uliobainika wakati wa utekelezaji wa sheria hiyo.

Miswada hiyo ilisomwa jana bungeni na makatibu mezani wa Bunge ikiwa ni siku ya mwisho ya Mkutano wa 10 wa Bunge la 12.

Ilibainishwa bungeni jijini hapa jana kuwa Muswada wa Sheria wa Marekebisho ya Sheria Mbalimbali za Fedha zipatazo nane una lengo la kuondoa upungufu ambao umejitokeza wakati wa utekelezaji wa baadhi ya masharti katika sheria hizo, ukisomwa kwa mara ya kwanza.

Sehemu ya tatu ya muswada inapendekeza marekebisho kwenye Sheria ya Huduma za Habari, Sura ya 229 ambapo kifungu cha 5(1) kinapendekezwa kufutwa kwa lengo la kumwondolea Mkurugenzi wa Idara ya Huduma za Habari, jukumu la uratibu wa matangazo yote ya serikali na pia kuiwezesha serikali kuwa na uhuru wa kuchagua chombo cha habari inachokitumia kwa ajili ya matangazo kwa kuzingatia nguvu ya ushindani kwenye soko.

Muswada huo pia unapendekeza kufutwa kwa kifungu cha 38(3) cha sheria hiyo kwa madhumuni ya kuongeza haki ya uhuru wa maoni.

Muswada unapendekeza marekebisho kwenye vifungu vya 50, 51, 53, 54, 55, 63 na 64 kwa madhumuni ya kuhakikisha waandishi wa habari wanafurahia haki yao ya uhuru wa maoni, haki ya kupata habari na uhuru katika kazi zao za uhariri bila kuwa na woga wa adhabu za kijinai.

Mapendekezo hayo ya marekebisho, pamoja na mambo mengine, yanalenga kuwaondoa waandishi wa habari katika makosa yanayohusiana na kashfa za kijinai, makosa ambayo kwa kawaida yanaangukia katika utaratibu wa mashauri ya madai.

Mapendekezo ya marekebisho ya vifungu hivyo yana lengo la kuondoa adhabu kwa wamiliki wa mitambo ya uchapishaji, ambao katika hali ya kawaida, hawana uwezo wa kudhibiti maudhui yanayochapishwa kwenye mitambo hiyo ya uchapishaji.

SPIKA, PM

Baada ya kusomwa bungeni, Spika wa Bunge, Dk. Tulia Ackson alisema miswada hiyo imesomwa kwa mara ya kwanza na itapelekwa kwenye kamati zinazohusika.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa akitoa hoja ya kuahirisha Bunge, aligusia miswada hiyo iliyowasilishwa bungeni.

Alisema Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria Mbalimbali wa Mwaka 2023 utasaidia kuboresha baadhi ya masharti na kuondoa upungufu uliobainika wakati wa utekelezaji wa masharti mbalimbali katika Sheria ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi pamoja na Sheria ya Huduma za Habari.

Pia alisema utaondoa upungufu kwenye Sheria ya Bohari ya Dawa; Sheria ya Mazishi ya Viongozi wa Kitaifa; Sheria ya Reli; Sheria ya Taasisi ya Utafiti wa Misitu Tanzania; Sheria ya Mamlaka na Majukumu ya Msajili wa Hazina na Sheria ya Kodi ya Ongezeko la Thamani.

Kadhalika, Majaliwa alisema Muswada wa Sheria ya Marekebisho ya Sheria ya Ubia Baina ya Sekta ya Umma na Sekta Binafsi wa Mwaka 2023 utasaidia kuboresha sheria hiyo na hivyo kuongeza kasi ya ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo.

Pia alisema kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kutaipunguzia serikali mzigo wa kibajeti na kukuza sekta binafsi.

# Bilioni 700/- kutumika utekelezaji miradi MSCL

**Na Vitus Audax, MWANZA**

KAMPUNI ya Meli (MSCL) inatarajia kuanza utekelezaji wa miradi mbalimbali ya usafirishaji ndani na nje ya nchi yenye thamani ya dola za Marekani milioni 300 (zaidi ya Sh. bilioni 700).

Hatua hiyo ni mwendelezo wa uboreshaji wa huduma za usafirishaji kwenye Ziwa Victoria na Ziwa Tanganyika.

Mkurugenzi Mkuu wa MSCL, Erick Hamisi alibainisha hayo juzi alipozungumza na waandishi wa habari kuhusu hatua ya pili ya ushushwaji wa meli ya MV. Mwanza Hapa Kazi Tu inayotarajiwa kushushwa majini hii kesho kwa ajili ya kuendelea na hatua ya mwisho ya umaliziaji.

Hamisi alisema katika mwaka huu wa fedha, kampuni hiyo inaendelea na mchakato wa kumpata mkadarasi kwa ajili ya utekelezaji wa miradi minne mikubwa ya ujenzi wa chelezo kubwa Ziwa Tanganyika, ujenzi wa meli mbili Ziwa Tanganyika pamoja na ujenzi wa meli nyingine moja ya mizigo Ziwa Victoria.

"Kupitia bajeti hii, tuna mpango wa kujenga meli tatu kubwa ambapo meli mbili zitajengwa mkoani Kigoma kwenye Ziwa Tanganyika, moja itakuwa meli ya mizigo pekee yenye uwezo wa kubeba tani 300 za mizigo na nyingine itakuwa ya abiria na mizogo yenye uwezo wa kubeba abira 600 na tani 400 za mizigo," alibainisha.

Hamisi aliongeza kuwa kwenye Ziwa Tanganyika itajengwa chelezo nyingine kubwa zaidi kuwahi kujengwa nchi za ukanda wa maziwa makuu ambayo itakuwa na uwezo wa kuweka meli mbili kwa wakati mmoja katika kipindi cha matengenezo, hivyo kusaidia ujenzi wa meli hizo kufanyika kwa wakati mmoja.

Kuhusu ushushwaji wa meli ya MV.Mwanza Hapa Kazo Tu kutoka kwenye chelezo kuingia majini, Hamisi alisema maandalizi yake yamekamilika na ulinzi unatarajiwa kuimarishwa zaidi na Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, Jeshi la Wananchi Tanzania pamoja na Jeshi la Polisi ili kukabiliana na tatizo lolote linaloweza kujitokeza wakati wa ushushwaji wa meli hiyo kubwa.

Kaimu Kamanda wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji Mkoa wa Mwanza, Kamila Laban alisema tayari wamepanga askari wa uokoaji majini na boti yao ili kusaidia katika shughuli za uokoaji.

Vilevile, alisema imeandaliwa mitungi ya kutosha ya kuzima moto pamoja gari la zimamoto kwenye eneo la tukio kuhakikisha hali ya usalama katika ushushwaji wa meli hiyo kubwa.

Baadhi ya wakazi wa Jiji la Mwanza walisema utekelezaji wa mradi huo ni fursa kwao hasa kwenye suala la usafiri na usafirishaji wa mizigo ndani na nje ya nchi."Kuwapo kwa meli hii kutatusaidia kupokea mizigo yetu kwa wakati kutoka katika Mkoa wa Kagera na nchi ya jirani ya Uganda, hivyo kufanya mzunguko wa biashara kuwa mkubwa tofauti na sasa," alisema mfanyabiashara Thomas Matitu.

# Tume haki jinai yaita wananchi kutoa maoni

**Na Maulid Mmbaga**

MWENYEKITI wa Tume ya Haki Jinai, Jaji Mkuu Mstaafu Othman Chande, amewataka Watanzania kutoa maoni katika kipindi cha siku 120 cha kusikiliza na kukusanya maoni ili kuwa na ripoti kamili itokanayo na maoni ya wananchi ambayo yanatekelezeka.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam, Chande alisema tume hiyo ilizinduliwa rasmi Januari 31, mwaka huu, na Rais Samia Suluhu Hassan kwa lengo la kufuatilia utendaji wa taasisi za haki jinai na kuainisha matatizo ambayo ni sugu na yanayojirudia.

Jaji Chande alisema tume hiyo ina majukumu mawili likiwemo la kufanya tathmini ya mfumo wa haki jinai kwa kuangalia utekelezaji wa wajibu wake kama kulinda jamii na mali zao, kudhibiti sheria na wahalifu.

"Jukumu lingine la tume ni kutathmini taasisi tano za haki jinai ambazo ni Jeshi la Polisi, Ofisi ya Taifa ya Mashtaka, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), Jeshi la Magereza na Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya," alisema.

"Lakini pia katika mfumo wa haki jinai kuna taasisi zingine zinahusika zikiwamo Mamlaka ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Mamlaka ya Usimamizi Wanyamapori, Misitu, na Mahakama ya Tanzania. Taasisi ni nyingi lakini mfumo wa haki jinai unatakiwa uwe mmoja na si miwili au mitatu," aliongeza.

Alibainisha kuwa wanachokiangalia pia ni kama taasisi hizo zinashirikiana na kufanya kazi kwa kutegemeana na kwamba lengo la Rais Samia ni kufanya maboresho makubwa ya haki jinai na taasisi husika kwa kuongeza weledi na ufanisi.

Aidha, alisema kusudio lingine la Rais Samia ni kusukuma gurudumu la haki jinai litende haki ili kukidhi matakwa ya watanzania, na kwamba wameshaanza kazi na tayari wameshafanya mazungumzo na Mkuu wa Jeshi la Polisi (IGP) Camillus Wambura, Kamishna wa Polisi Zanzibar, Mkuu wa Magereza Tanzania na Mkurugenzi wa Mashtaka Tanzania Bara na Zanzibar.

Hata hivyo, alimshukuru Rais Samia kwa kulipa uzito jambo hilo la haki jinai, na kwamba huo ni muendelezo wa dhamira ya kufanya maboresho ya kwenye mfumo wa haki jinai nchini.

"Hali halisi ni kwamba kuna mmomonyoko wa upungufu wa imani ya watanzania kwenye mfumo wa haki jinai na kwenye taasisi zinazotoa haki, kuna upungufu wa imani, ndiyo maana tunataka sisi kwenye mahojiano tupate taarifa zaidi.

"Na sisi nia yetu sio kukaa tu hapa hapana, tutatembelea mikoa 14 katika wilaya 30, na tunatoa wito kwa watanzania watoe mapendekezo yanayotekelezeka ili tuyafanyie kazi na tutoe ripoti kamili yenye mapendekezo yanayotekelezeka," alisema.

Alisema Watanzania wanaweza kutoa mapendekezo kupitia mitandao yote ya kijamii ya haki jinai na namba ya simu 0765010229.



Kaimu Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga ambaye ni Mkuu wa Mkoa wa Simiyu, Dk. Yahaya Nawanda (katikati), akikata utepe, kama ishara ya kukabidhi pikipiki 221 kwa Maofisa Ugani, mkoani humo jana, ili wakazitumie kutoa elimu ya kilimo cha kisasa kwa wakulima. **PICHA: MARCO MADUHU.**

# Serikali yawatoa hofu wananchi kuhusu hali upatikanaji chakula

**Na Romana Mallya,**
DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa, amewatoa hofu Watanzania kuwa hadi Januari 31, mwaka huu, hali ya upatikanaji wa chakula ilikuwa ya kuridhisha.

Aidha, ametoa wito kwa wakulima kutumia mifumo rasmi ya kuuza chakula ili kutokuwa katika hatari ya kukumbwa na upungufu siku za usoni.

Majaliwa aliyasema hayo jana bungeni jijini hapa wakati akiahirisha Mkutano wa 10 wa Bunge la 12.

"Nitoe wito kwa wakulima kujenga tabia ya kuhifadhi mazao yao badala ya kuuza yakiwa shambani pamoja na kutumia mifumo rasmi ya kuuza mazao ili kutokuwa katika hatari ya kukumbwa na upungufu wa chakula siku za usoni," alisema.

Pia aliwataka wakulima kutumia nyenzo rahisi zitakazoongeza thamani ya mazao yao badala ya kuuza yakiwa ghafi.

Majaliwa alisema kwa ujumla hali ya upatikanaji wa chakula imeendelea kuimarika ikichangiwa na uwapo wa ziada ya mazao ya chakula yasiyo ya nafaka yanayojumuisha jamii ya kunde, mhogo, ndizi, viazi vitamu, viazi mviringo, viazi vikuu na magimbi.

Alisema katika baadhi ya maeneo ya mikoa ya Kagera, Mwanza, Geita na Mara ambayo yamepata mvua za vuli kwa wakati, mahindi na maharage yamekomaa na kuendelea kuchangia upatikanaji wa chakula na hivyo, kuimarisha utengamano wa hali ya chakula. Pia alisema changamoto kubwa iliyopo sasa ni mabadiliko ya tabianchi, ambapo utabiri wa hali ya hewa umebainisha uwezekano wa mvua chini ya wastani kunyesha kwenye maeneo mengi nchini.

"Hali hiyo inaweza kuathiri uzalishaji si tu katika sekta ya kilimo bali pia upatikanaji wa nishati ya umeme, maji, mauzo nje, ukuaji wa uchumi, mapato ya mtu mmoja mmoja, kampuni na Serikali kwa ujumla.

"Serikali katika kukabiliana na hali hii imeendelea kuchukua hatua zikiwamo kutoa elimu ya ugani kwa kilimo cha mazao ya chakula na biashara, kuimarisha kilimo cha umwagiliaji sambamba na kutoa ruzuku ya pembejeo hususan mbolea ili kuongeza tija na uzalishaji kwenye mazao ambapo hadi Desemba, 2022 tani 175,829.3 zenye thamani ya Sh. bilioni 192.5 zimesambazwa," alisema.

Kuhusu hali ya mazao katika maeneo yaliyopata mvua za vuli kwa wakati (Septemba na Oktoba), alisema ni nzuri na yamefikia hatua za kuchanua, kubeba na kukomaa na baadhi ya maeneo wakulima wameanza kuvuna na kuhifadhi. Alisema katika maeneo ambayo mvua zilianza kwa kuchelewa, zimeendelea kunyesha na mazao yako katika hatua ya kukua, kuchanua na kubeba.

Majaliwa alisema hali ya utekelezaji wa bajeti ya Serikali kwa mwaka 2022/2023 katika nusu ya kwanza, Julai hadi Desemba, 2022, imeendelea kuimarika.

" Katika kipindi hicho, ridhaa ya matumizi iliyotolewa ilikuwa Sh. trilioni 19.46, sawa na asilimia 91.7 ya lengo. Kati ya kiasi hicho, Sh. trilioni 12.29 ni fedha za matumizi ya kawaida, sawa na asilimia 93.2 ya lengo na Sh. trilioni 7.17 ni fedha za maendeleo, sawa na asilimia 95.1 ya lengo," alisema.

Pia alisema mapato ya ndani na makusanyo yamekuwa ya kuridhisha ambapo katika kipindi cha Julai hadi Desemba, 2022 mapato ya ndani yakijumuisha mapato ya halmashauri yalifikia Sh. trilioni 13.40 sawa na asilimia 96.6 ya lengo, Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilikusanya Sh. trilioni 11.68 sawa na asilimia 98.1 ya lengo.

'Mapato yasiyokuwa ya kodi yalikuwa Sh. trilioni 1.26, sawa na asilimia 86.3 ya lengo na mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa yalifikia Sh. bilioni 458.6, sawa na asilimia 89.7 ya lengo la kipindi hicho," alisema.

Utekelezaji wa bajeti ya Serikali ya mwaka 2022/2023 kwa kipindi cha nusu mwaka, alisema umewezesha mafanikio mbalimbali ikiwamo upatikanaji wa fedha kwa ajili ya kugharamia shughuli mbalimbali, ukuaji chanya wa uchumi wa asilimia 5.2 na kuongezeka kwa ufanisi katika ukusanyaji wa mapato ya kodi ambapo ukuaji ulifikia asilimia 12.2.

Alizielekeza Halmashauri zenye mapato yasiyolindwa chini ya Sh. bilioni mbili (Kundi C), kuhakikisha zinatenga angalau asilimia 20 kwa ajili ya miradi ya maendeleo ikijumuisha asilimia 10 ya mikopo ya wanawake, vijana na watu wenye ulemavu.

**UJENZI MADARASA**

Alisema hadi Februari 3, mwaka huu, vyumba vya madarasa 7,874 katika shule za sekondari sawa na asilimia 98.43 vilikamilika na vyumba vya madarasa 126 sawa na asilimia 1.57 viko katika hatua mbalimbali za umaliziaji, hivyo kuwezesha wanafunzi 1,076,037 waliofaulu kujiunga kidato cha kwanza.

Pia alisema hadi Februari 3, mwaka huu, wanafunzi 1,363,320 wa darasa la awali waliandikishwa wakiwamo wenye mahitaji maalum 2,944.

"Wanafunzi wote wa darasa la awali walioandikishwa ni sawa na asilimia 100.18 ya lengo la kuandikisha wanafunzi 1,360,737. "Wakuu wa Mikoa hakikisheni wanafunzi wote wenye rika lengwa wanaandikishwa kwa ajili ya darasa la awali na darasa la kwanza kama ambavyo nimeainisha hapo nyuma," aliagiza.

Pia alisema wakulima waliolima maeneo ya hifadhi baada ya kuvuna wote watapaswa kuondoka mara moja na kwamba serikali itaendelea kutoa elimu kuhusu umuhimu wa uhifadhi na utunzaji wa vyanzo vya maji.

Alisema tathmini iliyofanywa na timu ya wataalamu kwenye mikoa 26 imebainisha kuwa ardhi yenye ukubwa wa ekari 1,630,639 imerejeshwa kwa wananchi.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

## Kila la heri Simba, Yanga katika michuano ya CAF

**WAWAKILISHI** wa Tanzania waliobakia katika mashindano yanayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), Simba na Yanga zote za jijini, Dar es Salaam wanatarajia kushuka ugenini kuanza kupeperusha bendera ya nchi kwenye michuano ya kimataifa.

Yanga, mabingwa watetezi na vinara wa Ligi Kuu Bara wao wanashiriki hatua ya makundi katika mashindano ya Kombe la Shirikisho Afrika wakati Simba yenyewe itapeperusha bendera ya Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

Wekundu wa Msimbazi wao wanatarajia leo kushuka kwenye Uwanja wa Nongo- Stade General Lansana Conte ulioko katika mji wa Conakry, Guinea kuwavaa wenyeji Horoya AC wakati US Monastir ya Tunisia itawakaribisha Yanga kesho katika jiji la Tunis.

Baada ya mechi hizo za kwanza za hatua ya makundi, wawakilishi hao watarejea nyumbani, Yanga itawaalika TP Mazembe kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na Raja Casablanca ya Morocco itawafuata Simba, mechi zote zikipangwa kuchezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam wikendi ijayo.

Tunaamini benchi la ufundi la timu hizo mbili, zimefanyia kazi mapungufu yote waliyonayo kupitia mechi za Ligi Kuu Bara, michuano ya Kombe la FA na michezo mbalimbali ya kirafiki ili kuimarisha vikosi vyao kuelekea mashindano hayo ya CAF yaliyoko mbele yao.

Pia kutokana na teknolojia na soka la kisasa, ni wazi, Simba na Yanga zilituma watu mapema huko Guinea na Tunisia ili kuwapeleleza wapinzani wao pamoja na kutumia picha za video kwa malengo ya kujipanga vyema kuwakabili na hatimaye kupata matokeo chanya.

Ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kusonga mbele na kufikia malengo, Simba na Yanga zinatakiwa kucheza kwa bidii na wachezaji wao wanatakiwa kuamini uwezo wa kupata ushindi au sare ugenini wanao, kama ambavyo timu za Waarabu na Afrika Magharibi walivyokuwa wanapata miaka ya nyuma.

Usajili mzuri wa wachezaji uliofanyika pamoja na makocha wenye uwezo wa juu walioajiriwa na timu hizo kongwe hapa nchini, ni dalili njema za kujipandisha daraja na kuonyesha wako tayari kwa vita ya kusaka matokeo mazuri kwenye michuano hiyo inayofanyika kila mwaka hapa barani Afrika. Wachezaji wanatakiwa kujituma ili kujiongezea thamani, kwa sababu kupitia michuano hiyo, mawakala kutoka nchi mbalimbali za Afrika na Ulaya hufuatilia, hivyo ni sehemu nyingine ya wao kujiweka sokoni kuzivutia klabu za nje na hatimaye kuwasajili.

Makocha pia wanahitaji kupata matokeo chanya ambayo yatawafanya wao kupata heshima na kulipwa kiasi kikubwa cha posho kutokana na kuzifikisha timu hizo katika hatua ya kuanzia robo fainali, nusu fainali au fainali. Simba na Yanga huu ni wakati wenu wa kuipa nchi heshima kwa kufanya vizuri katika michezo yote, ikiwezekana pia mjipange kupata ushindi ugenini ili kujirahisishia kazi ya kusonga mbele na kuacha kupigia hesabu michezo ya nyumbani peke yake.

Tunaamini katika kufikia malengo ya kufanya vizuri, kila mtu anayehusika na timu ametekeleza majukumu yake kwa kiwango cha juu na kutosikia utetezi wowote baada ya mechi hizo za kwanza kumalizika, lakini pia maandalizi ya michezo inayofuata yakiwa yanakaribia ukingoni.

Mbali na timu kujiandaa vyema kiufundi na kisaikolojia, Nipashe inapenda kuwakumbusha mashabiki wa soka nchini kuacha tabia za kuwasaidia wageni kwa sababu tu wanakutana na mtani wako, tuache vitendo hivyo na badala yake tuweke mbele uzalendo kwa faida ya Tanzania.

Endapo Simba na Yanga zitafanya vyema katika mechi zake za hatua ya makundi, ni wazi zitaiongezea Tanzania pointi na hatimaye msimu ujao kuendelea kupata nafasi nne, na kama 'utamaduni' wa kuwapa nguvu wageni utaendelea, ifahamike si kwamba utamkomoa mtani wako, bali utaiumiza nchi kwa kupoteza nafasi nyingi za uwakilishi kwenye michuano hiyo ya CAF. Tunaamini kila timu ikiwekeza vyema nguvu zake zaidi ya inavyofanya wakati Simba na Yanga zinavyokutana, hakika zitapata matokeo chanya na ndoto za kucheza hatua ya nusu fainali, fainali au kubeba ubingwa wa Afrika zitatimia.

Kila la heri Simba SC na Yanga katika kupeperusha vyema bendera ya Tanzania. Kazi iendelee.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwangowango

## Uzalendo muhimu kuelekea 'vita' michuano ya kimataifa

**WAKATI** wawakilishi wa Tanzania kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika, Simba leo wapo nchini Guinea kucheza dhidi ya Horoya, Yanga yenyewe kesho watakuwa nchini Tunisia kuwakabili US Monastir ya huko kwenye mashindano ya Kombe la Shirikisho.

Timu zote za Tanzania zitakuwa zinacheza mechi za kwanza hatua ya makundi zikiwa, ugenini, Simba ikiwa Kundi C na Yanga ipo Kundi D.

Zinakwenda kucheza mechi hizo zikiwa zimejiimarisha na kwa mara ya kwanza baadhi ya mashabiki wanazitabiria ushindi au kutoka sare katika michezo yao.

Si jambo lililozoeleka, mashabiki wa Simba na Yanga kuwa na matumaini ya ushindi zinapokwenda kucheza ugenini, badala yake wanachokuwa wanasubiri ni kudra tu za Mwenyezi Mungu na si uwezo wa vikosi vyao.

Kwa sasa wawakilishi wote wa Tanzania wamesheheni vikosi ambavyo kama makocha wanachanga karata zao sawa sawa vinaweza kupata ushindi dhidi timu nyingi tu barani Afrika.

Wakazi timu hizo zinakwenda kucheza mechi hizo, binafsi naziombea zifanye vyema si michezo hiyo tu, bali kuweza kupita kwenye hatua ya makundi na kutinga robo fainali.

Itakuwa ni furaha iliyoje, Simba ikisonga mbele hatua ya makundi na kufika hatua ya robo fainali, huku Yanga nayo ikipita kwenye kundi lake na kusonga mbele.

Si tu klabu hizo zitalinda nafasi zile nne zilizopo kwa Tanzania, lakini pia zitalifanya soka la hapa nchini lizidi kuvutia wengi barani Afrika, na msimu ujao kupanda kutoka nafasi ya tano iliyopo.

Hata hivyo, kama Simba na Yanga zinataka kusonga mbele kwenda hatua hiyo, kuna mambo ambayo wanapaswa kuachana nayo.

Tabia hii ilijengeka miaka michache nyuma ya kwenda kupokea timu ngeni uwanja wa ndege.

Kwa bahati mbaya sana, hata baadhi ya waandishi wa habari na wachambuzi walishindwa kulikemea na kulitengenezea mazingira fulani ili kuonekane ni la kawaida.

Mashabiki wanavaa jezi ya timu yao, halafu wanakwenda uwanja wa ndege kuipokea timu ambayo inacheza dhidi ya timu nyingine hapa hapa Tanzania na kuonyesha kuwaunga mkono ni jambo la hovyo ambalo limewahi kutokea kwenye nchi hii.

Wale ambao wanatetea kitu kama hiki wanasema huwezi kumlazimisha shabiki kupenda timu fulani, hilo lipo.

Ni kweli kabisa huwezi kuwalazimisha mashabiki wa Yanga kuishangilia Simba, au kinyume chake, lakini wakafanye hivyo uwanjani ambapo soka linachezwa.

Kule halazimishwi mtu, lakini tunachosema hapa kuonyesha kwa asilimia zote kubwa mashabiki wa Tanzania kwenda kuwapokea wageni na kuwapa mikakati ya ushindi dhidi ya timu ya hapa huo si uanamichezo.

Shabiki wa Simba anatakiwa akae tu atulie wakati wapinzani wa Yanga wamewasili. Anachotakiwa yeye ni kwenda uwanjani tu kuwashangilia kwa ajili ya kudumisha utani na si kitu kingine.

Niseme kweli tu kuwa kitendo cha mashabiki wa Yanga ambao walijenga tabia ya kwenda kuwapokea wapinzani watakaocheza dhidi ya Simba katika michuano ya kimataifa, ilikuwa inaleta uhasama badala ya utani.

Kama vile haitoshi kulikuwa na video fupi na meseji ambazo wageni walikuwa wakiahidiwa kusaidiwa na kutahadharishwa baadhi ya mambo wanapofika nchini.

Na kwa bahati nzuri tu Simba ilikuwa ikishinda mechi zake nyingi, lakini kama ingekuwa kinyume chake sijui ingekuwaje.

Kwa bahati nzuri sasa zote zipo kimataifa, sitarajii mashabiki wafanye kama walivyokuwa wakifanya huko nyuma. Nadhani sasa kila mmoja atakuwa 'bize' na timu yake.

Nadhani sasa imefika wakati kuachana na tabia hiyo kwa manufaa ya taifa. Timu zinapambana kwa ajili ya kulibeba taifa kwenye soka kimataifa. Ni ile ile tu hadithi ya watu wanaojenga nyumba moja, lakini wanagombea fito.

Sababu ni eti mmoja anataka kumcheka mwenzake, au kumfanya asishinde kwa sababu wanaongea sana.

Kuchekana ipo, subiri afungwe, lakini siyo kufanya juhudi au mikakati ili mtani wako afungwe umcheke.

Huu si mpira kabisa.

Simba na Yanga zinafanya vyema kwenye michuano hii kama tabia hiyo itaachwa na kuliacha 'boli kutembea uwanjani' na si kupokeana uwanja wa ndege na kufanya mambo ya kukwazana na kufanyiana hujuma.

# Majaliwa: PEPFAR imepunguza maambukizi mapya VVU nchini

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amesema Tanzania imefanikiwa kupunguza maambukizi mapya ya Virusi vya Ukimwi (VVU) kwa asilimia 58 kutoka 130,000 mwaka 2003 hadi 54,000 mwaka 2021 kupitia Mfuko wa Dharura wa Rais wa Marekani wa Kupambana na UKIMWI (PEPFAR).

Amesema mfuko huo ambao umeleta mabadiliko makubwa katika mapambano dhidi VVU, pia umesaidia kupunguza vifo kwa asilimia 76 kutoka 120,000 mwaka 2003 hadi 29,000 mwaka 2021.

Aliyasema hayo jana wakati wa hafla ya maadhimisho ya miaka 20 ya mafanikio katika mapambano dhidi ya VVU/UKIMWI yaliyowezeshwa na PEPFAR jijini Dar es Salaam.

Majaliwa alisema Serikali ya Tanzania itaendelea kuunga mkono mpango huo katika kujenga miundombinu ya afya, kutoa mafunzo, kutoa vifaa vya uchunguzi na vifaa vya kinga binafsi, na kuanzisha mifumo ya kufuatilia maambukizi.

"Serikali ya Tanzania inafahamu kwamba Serikali ya Marekani ni mshirika mkubwa katika kukabiliana na VVU nchini, ikiwa imewekeza zaidi ya dola za Marekani bilioni 6.6 kwa ajili ya kukabiliana na janga hilo," alisema.

Majaliwa alisema PEPFAR kwa sasa inasaidia zaidi ya watu milioni 1.5 wanaoishi na VVU (WAVIU) kwenye matibabu kupitia mpango wa kuokoa maisha wa ARV ambapo kabla ya kuanzishwa kwa mpango huo, WAVIU wasiozidi 1,000 ndio walikuwa kwenye Tiba ya Kupambana na VVU.

Alisema Serikali ya Tanzania inajivunia kushirikiana na Serikali ya Marekani kupitia PEPFAR kufikia malengo ya 95/95/95 ifikapo mwaka 2025.

"Hivi sasa kupitia mpango wa PEPFAR tunatekeleza utafiti wa athari za VVU Tanzania kwa mwaka 2022-2023 ambao unakusudiwa kutoa taarifa muhimu katika kuandaa mikakati ya kuzuia maambukizi mapya na kuhakikisha watu wanajua hali zao za VVU," alisema.

Mkurugenzi Mkazi wa PEPFAR Tanzania, Jessica Greene alisema licha ya mafanikio yaliyopatikana, bado kuna kazi kubwa ya kuhakikisha upatikanaji wa huduma unaongezwa kwa wasichana, wanawake vijana, watoto na makundi ya jamii yaliyo katika hatari kubwa zaidi ya kuambukizwa VVU.



Mkazi wa Majohe jijini Dar es Salaam, Sea Tumba, akichangia hoja, katika mafunzo ya jinsi ya kuripoti vitendo vya ukatili, yaliyoandaliwa na Kituo cha Sauti ya Jamii Kipunguni kwa ushirikiano na Taasisi ya Haki Kiganjani, juzi. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Vyuo vikuu vyapewa angalizo ubora TEHAMA

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia amevitaka vyuo vikuu nchini kuandaa programu za Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEHAMA) zinazoendana na maendeleo ya dunia katika kukidhi soko la ajira nchini.

Dk. Francis Michael alitoa rai hiyo juzi wakati anafungua kongamano la siku mbili kuhusu uvumbuzi lililoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na Japan katika progamu hizo kwa sababu suala la TEHAMA linachangia kuleta maendeleo ya haraka kwenye taifa.

"Vyuo vikuu lazima vije na programu ambazo zinaendana na maendeleo ya TEHAMA ya duniani kwa sababu suala la TEHAMA lina maendeleo ya haraka.

"Tunatakiwa tuwe na programu ziazoendana, vinginenvyo taasisi zetu na vyuo vyetu vitakuwa vinatoa wanafunzi ambao wanakosa ushindani katika soko la ajira," alisema Dk. Michael.

Mwakilishi Mkuu wa JICA nchini, Yamamura Naofumi alisema Tanzania na Japan zimekuwa na ushirikiano wa muda mrefu katika masuala ya kijamii na kiuchumi.

"Shughuli za JICA kwa muda mrefu zimejumuisha utoaji wa ushirikiano wa kiufundi, misaada ya ruzuku na mikopo ya masharti nafuu kusaidia miradi mingi ya maendeleo.

"Shughuli hizi ni kwa mujibu wa ombi la serikali kwa lengo la kuunga mkono juhudi za Watanzania kujisaidia katika kuinua maisha yao na kuondoa umaskini," alisema Naofumi.

Naibu Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. Boniventure Rutinwa alisema kongamano hilo ni sehemu ya uanzishwaji wa programu ya mafunzo yatakayoiwezesha Tanzania kupitia UDSM kujifunza kutoka Japan.

"Japan ina sifa ya pekee duniani, ni nchi ambayo imeendelea na imeweza kufikia viwango vya kwanza vya maendeleo bila kuiga na kufata mbinu za watu wa magharibi na wameweza kuendelea bila kupoteza utamaduni wao," alisema.

# Wafungwa jela miaka 30 kwa unyang'anyi

**Na Stevie Chindiye,** TUNDURU

WATU sita wamehukumiwa kutumikia kifungo cha miaka 30 jela kila mmoja baada ya kupatikana na hatia katika kesi ya unyang'anyi wa kutumia silaha.

Waliohukumiwa kutumikia vifungo hivyo ni Mohammed Hassan (38), Lujanga Said (26), Said Mohammed (25), Mohammed Ally (46), Ajana Timamu (23) na Issa Namwewe wote wakazi wa kijiji cha Ligunga, wilayani Tunduru.

Sambamba na kuhukumiwa adhabu hiyo, mahakama pia imeamuru kutaifishwa na serikali pikipiki aina ya SLG yenye namba za usajili T743 BXK baada ya kuthibika kuwa ilikuwa ikitumika kwenye matukio ya uporaji wa mali za watu.

Hukumu hiyo ilitolewa juzi na Hakimu Mkazi mwandamizi Mfawidhi wa Mahakama ya Wilaya ya Tunduru, Honorious Kando, huku akibainisha kuwa uamuzi huo umefikiwa baada ya kujiridhisha na ushahidi uliotolewa na upande wa Jamhuri pasina kuacha shaka yoyote kuwa washtakiwa walifanya kosa hilo.

"Mahakama inatoa adhabu hii baada ya kujiridhisha bila kutia mashaka yoyote na ushahidi uliotolewa ukiongozwa na mwendesha mashitaka, Mkaguzi Msaidizi wa Polisi Philipo Zengo huku ikizingatiwa rekodi za nyuma za uhalifu wa makosa hayo yaliyotolewa na waendesha mashtaka," alisema Hakimu Kando.

Awali akisoma shitaka hilo namba 43 la mwaka 2022 mbele ya Hakimu Kando, mwendesha mashtaka Inspekta Zengo alidai kuwa washtakiwa hao kwa pamoja walitenda kosa hilo Februari 2, 2022.

Zengo alidai kuwa washtakiwa hao walitenda kosa hilo la unyang'anyi kinyume cha kifungu cha sheria namba 287 A cha Sheria ya Kanuni ya Adhabu sura ya 16 kama ilivyo fanyiwa marejeo mwaka 2022. Alidai kuwa kitendo hicho kilichofanywa na washtakiwa hao, kimemfanya mlalamikaji kushindwa kutimiza majukumu yake ya kuihudumia familia yake.

Kwa mujibu wa Zengo, washtakiwa hao walikamatwa baada ya kupora simu aina ya Tecno pamoja na nguo mbalimbali, vyote vikiwa na jumla ya thamani ya Sh. 200,000 mali ya Desderia Kirian mkazi wa Masasi baada ya kumtishia kumjeruhi kwa kumkata mapanga pamoja na kumpiga na nondo walizokuwa nazo.

Alidai kuwa katika tukio hilo, washtakiwa walivamia gari la mizigo wakiwa wanatumia pikipiki aina ya SLG yenye namba za usajili T743 BXK na kutumia mbinu ya kutishia kuwadhuru kwa kutumia silaha za jadi watu waliokuwa katika gari hilo na kufanikisha azma yao.

Baada ya mahakama kuwatia hatiani, Zengo aliiomba mahakama kutoa adhabu kali kwa washtakiwa ili liwe fundisho kwa watu wengine ambao wamekuwa na tabia za aina hiyo.

Alidai kuwa kutokana na kushamiri kwa matukio hayo, washtakiwa hao wamekuwa wakisababisha kuporomoka kwa uchumi wa wamiliki wa mali hizo.

Wakitoa utetezi mbele ya hakimu, washtakiwa waliiomba mahakama kuwapatia adhabu ndogo kwa vile hilo ni kosa lao la kwanza na kwamba wanategemewa na familia wazazi na watoto ambao wanawasomesha.

# Mkuu wa wilaya atangaza msako kwa watoto wasioripoti kidato cha kwanza

**Na Steven William,**
NACHINGWEA

Mkuu wa Wilaya ya Nachingwea, Mohamed Moyo, ameanza kazi kwa kutangaza msako wa nyumba kwa nyumba wa wanafunzi ambao hawajaripoti shuleni kuanza kidato cha kwanza mwaka huu ili wajulikane wako wapi.

Moyo alitoa agizo hilo juzi mjini hapa akiwa katika sehemu ya ziara aliyoianzisha ya kijiji kwa kijiji kwa ajili ya kujitambulisha kwa wananchi na viongozi wa vyama na serikali baada ya kuripoti akitokea Iringa. Moyo alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Iringa.

Alisema suala la watoto kuripoti shuleni ameshatoa maelekezo wakati wa makabidhiano ya ofisi na mtangulizi wake kwa maofisa tarafa ili kubaini watoto ambao walipangwa kuwapo shuleni na hawajaripoti na mahali waliko. Moyo pamoja na kutangaza hilo, aliwakumbusha wazazi na walezi ambao watoto wao wamechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza kuhakikisha wanafanya hivyo ndani ya mwezi mmoja na baada ya hapo hatua zitachukuliwa.

Alisema kama maagizo yake yatakuwa yameshindikana, ataanza msako mwenyewe pamoja na watendaji ili kuhakikisha wazazi na walezi walioshindwa kupeleka watoto shuleni wanakamatwa. Pia aliwaonya wazazi ambao wamewaozesha watoto wao badala ya kwenda shuleni kwamba dawa yao inachemka.

Mkuu huyo wa wilaya alisema Rais Samia Suluhu amejenga madarasa mengi katika shule za sekondari nchini kutumia fedha za UVIKO - 19 kwa lengo la kuhakikisha watoto wanasoma kuanzia darasa la kwanza mpaka kidato cha sita bure lakini baadhi ya wazazi hawataki kuwapeleka watoto wao shule.

"Haya ni mapambano na mapambano ni vita na vita si lelemama. Haki na ustawi wa mtoto lazima usimamiwe, hivyo mtoto akizaliwa ni mali ya serikali. Mzazi yeyote ambaye atasababisha mwanawe kutokwenda shuleni kwa kisingizio chochote, hatavumiliwa," alisema Moyo.

Katika hatua nyingine, Moyo aliwaomba viongozi na wananchi wa wilaya ya Nachingwea kumpa ushirikiano katika utendaji kazi ili kuiletea maendeleo wilaya hiyo katika sekta mbalimbali.

Alisema kuwa anaomba ushirikiano mkubwa kutoka kwa viongozi wenzake watumishi, madiwani, viongozi wa Chama, wananchi na wazee wa wilaya hiyo ili kuhakikisha anafanikisha wilaya hiyo inakuwa kiuchumi na kukuza maendeleo kwa wananchi. Aidha, Moyo aliwahakikishia wananchi wa wilaya hiyo kuwa nao bega kwa bega na milango iko wazi wakati wowote kusikiliza kero zao.



Waziri Mkuu, Kasimu Majaliwa akiagana na baadhi ya wabunge, baada ya kuahirisha shughuli za Bunge, jijini Dodoma jana hadi mwezi Aprili mwaka huu. **PICHA: IBRAHIM JOSEPH**

# PM ataka uwajibikaji udhibiti maafa

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI MKUU Kassim Majaliwa amezitaka sekta zote zinazohusika na utekelezaji wa shughuli za usimamizi wa maafa, idara au taasisi zenye jukumu la kisheria la kutekeleza kazi hiyo kuwajibika kikamilifu pindi maafa yanapotokea.

Amesema pamoja na uwapo wa sera na sheria ya usimamizi wa maafa na nyaraka alizozindua ambazo zimelenga kuimarisha mifumo ya uwajibikaji kwa kila sekta, ushirikiano unahitajika katika kutekeleza afua za ustahimilivu na kuzuia maafa.

Majaliwa aliyasema hayo juzi wakati akizindua nyaraka za usimamizi wa maafa katika Ukumbi wa Hazina, jijini Dodoma. Nyaraka zilizozinduliwa ni pamoja na Mpango wa Taifa wa Kujiandaa na kukabiliana na Maafa (2022).

Zingine ni Mkakati wa Taifa wa Mawasiliano Wakati wa Maafa (2022), Mpango Mkakati wa Taifa wa Afya Moja (2022-2027), Mkakati wa Taifa wa Usimamizi wa Maafa (2022-2027) na Mwongozo wa Taifa wa Kupambana na Vitendo vya Kihalifu katika Bahari na Maziwa Makuu (2022).

Alisema miongozo na mipango hiyo ya usimamizi wa maafa inatoa jukumu kwa wizara na mamlaka za serikali za mitaa, hivyo taasisi pamoja na wadau wengine kuandaa mipango kazi na taratibu za usimamizi wa maafa pamoja na namna ya kushughulikia dharura pindi inapojitokeza.

Waziri Mkuu alisema nchi bado ina uwezo wa kudhibiti majanga yanayosababishwa na shughuli za kibinadamu, hivyo wahusika wawajibike katika kuelimisha umma wa Watanzania namna ya kukabiliana na majanga na kusimamia kikamilifu utekelezaji wa nyaraka hizo.

"Nitoe rai kwa Watanzania wenzangu, tuwe sehemu ya watendaji wakati wa dharura zinapojitokeza badala ya kusubiri tuanze kulaumu.

Wale wenye nguvu na uwezo wa kusaidia wajitokeze kuunga mkono jitihada za serikali badala ya kuwa watazamaji mfano ilipotokea ajali ya ndege wananchi walijitokeza kusaidia," alisema.

Waziri Mkuu aliwahakikishia wananchi kuwa serikali itaendelea kuimarisha mbinu na mikakati ya makusudi ya udhibiti wa athari zitokanazo na maafa pamoja na usimamizi wa utekelezaji wa sera, sheria na mikakati ya usimamizi wa maafa.

Pia alizielekeza wizara, tawala za mikoa na serikali za mitaa na taasisi zingine zitenge fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli za usimamizi wa maafa katika maeneo yao.

"Waheshimiwa mawaziri mliopo hapa, makatibu wakuu, makatibu tawala wa mikoa na wakurugenzi wa halmashauri, nendeni mkasimamie kikamilifu bajeti katika maeneo yenu ili kuwezesha usimamizi wa maafa," alisisitiza.

Majaliwa alisema viongozi hao wanatakiwa kutenga rasilimali kabla ya kutokea kwa maafa na kwa kufanya hivyo watakuwa wamejijengea uwezo wa kukabiliana na maafa hayo, pia sekta zote zilizopewa majukumu ya kusimamia maafa zihakikishe zinaratibu upatikanaji wa msaada wa kitaalamu na vifaa vya utafutaji na uokoaji.

# Vyuo vikuu vyapewa angalizo ubora TEHAMA

**Na Mary Geofrey**

KATIBU Mkuu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia amevitaka vyuo vikuu nchini kuandaa programu za Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEHAMA) zinazoendana na maendeleo ya dunia katika kukidhi soko la ajira nchini.

Dk. Francis Michael alitoa rai hiyo juzi wakati anafungua kongamano la siku mbili kuhusu uvumbuzi lililoandaliwa na Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Japan (JICA) kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

Alisema serikali itaendelea kushirikiana na Japan katika progamu hizo kwa sababu suala la TEHAMA linachangia kuleta maendeleo ya haraka kwenye taifa.

"Vyuo vikuu lazima vije na programu ambazo zinaendana na maendeleo ya TEHAMA ya duniani kwa sababu suala la TEHAMA lina maendeleo ya haraka.

"Tunatakiwa tuwe na programu ziazoendana, vinginenvyo taasisi zetu na vyuo vyetu vitakuwa vinatoa wanafunzi ambao wanakosa ushindani katika soko la ajira," alisema Dk. Michael.

Mwakilishi Mkuu wa JICA nchini, Yamamura Naofumi alisema Tanzania na Japan zimekuwa na ushirikiano wa muda mrefu katika masuala ya kijamii na kiuchumi.

"Shughuli za JICA kwa muda mrefu zimejumuisha utoaji wa ushirikiano wa kiufundi, misaada ya ruzuku na mikopo ya masharti nafuu kusaidia miradi mingi ya maendeleo.

"Shughuli hizi ni kwa mujibu wa ombi la serikali kwa lengo la kuunga mkono juhudi za Watanzania kujisaidia katika kuinua maisha yao na kuondoa umaskini," alisema Naofumi.

Naibu Makamu Mkuu wa UDSM, Prof. Boniventure Rutinwa alisema kongamano hilo ni sehemu ya uanzishwaji wa programu ya mafunzo yatakayoiwezesha Tanzania kupitia UDSM kujifunza kutoka Japan.

"Japan ina sifa ya pekee duniani, ni nchi ambayo imeendelea na imeweza kufikia viwango vya kwanza vya maendeleo bila kuiga na kufata mbinu za watu wa magharibi na wameweza kuendelea bila kupoteza utamaduni wao," alisema.





## Nyumba milioni 3 zinahitajika nchini

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

MKURUGENZI Mtendaji wa Shirika la Watumishi Housing Investments, Dk. Fred Msemwa amesema mahitaji ya nyumba nchini ni milioni tatu huku Mkoa wa Dar es Saalam pekee ukihitaji nyumba 400,000.

Dk. Msemwa alibainisha hayo juzi jijini hapa alipotoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali pamoja na mipango ya badaye ya shirika hilo.

Alisema kutokana na mahitaji ya nyumba yaliyopo nchini, shirika hilo limekuwa likijikita zaidi katika ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa ajili ya makundi yote nchini.

"Takwimu zinaonyesha kuwa kati ya Watanzania 100 ni 15 pekee ndiyo wenye uwezo wa kununua nyumba ya bei ya kuanzia Sh. milioni 25 na kuendelea, hivyo kutokana na hali hiyo sisi tumeamua kuwa na miradi ya ujenzi wa nyumba za gharama nafuu kwa ajili ya watu wote," alisema.

Aliongeza kuwa kutokana na umuhimu wa nyumba, shirika hilo limekuwa likitekeleza miradi mbalimbali ya nyumba za gharama nafuu kwenye mikoa mbalimbali nchini.

"Kuna uhusiano mkubwa kati ya kuwa na nyumba bora na kuwa na fedha, hivi vitu vinategemeana, hivyo kupitia Watumishi Housing Investments tumeanzisha mfuko wa Faida Fund ambao utayalenga makundi yote ya kijamii," alifafanua.

Alisema lengo kuu la kuanzisha mfuko huo ni kuwawezesha wananchi kiuchumi kupitia uwekezaji wa pamoja.

"Wananchi wa kawaida wakiwamo watoto, wakulima, wavuvi, watumishi wa umma, wafanyakazi, kampuni na taasisi sasa wanawekeza kwenye mfuko huu mpya wa Faida Fund," alisema.

Alisema mfuko huo umeanzishwa chini ya Sheria ya Masoko ya Mitaji na Dhamana Sura 79, akibainisha kuwa mfuko huo wa uwekezaji wa pamoja ambao umekuja sokoni kuongeza nguvu na kuchochea tabia ya kuwekeza kwa lengo kuu la kuwawezesha Watanzania kiuchumi kwa kukuza mitaji yao.

Alisema mauzo ya awali ya vipande vya Faida Fund yalianza Novemba Mosi mwaka jana na kuisha Desemba 31, 2022 na bei ya kipande ilipanda thamani kutoka Sh. 100 na kuwa 3,400 hivyo kutoa gawio kwa asilimia 34.

Vilevile, alisema Watumishi Housing Investment inategemea kuwa na miradi mipya ya ujenzi katika mwaka wa fedha 2022/2023.

Alisema miradi hiyo ni pamoja na ule wa Kawe Apartment, Dodoma, Gezaulole Housing Project, mradi wa viwanja Arusha na nyumba za watumishi wa halmashauri mpya.

# Majaliwa ataka bajeti na uwajibikaji katika maafa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

WAZIRI Mkuu, Kassim Majaliwa amezitaka sekta zote zinazoshughulikia maafa, kutenga bajeti na ziwajibike pindi majanga yanapotokea.

Pia amezitaka kuandaa vifaa kwa ajili ya kukabiliana na majanga mbalimbali pindi yanapotokea.

Alitoa maagizo hayo juzi wakati akizindua nyaraka za maafa katika hafla iliofanyika jijini hapa.

Alisema Ofisi ya Waziri Mkuu tayari imeanza kutoa elimu na vifaa kwenye ukanda wa Ziwa Victoria kwa wavuvi ambao wako maeneo hayo.

Alisema lengo la kufanya hivyo ni pamoja na kutaka kuwajengea uwezo ili pindi dharura kama hizo zinapotokea, jamii itoe msaada wa uokoaji katika majanga mbalimbali yanayotokea.

Alisema wameanzia huko lakini wataendelea na sehemu nyingine kwa lengo kujengeana uwezo ili tatizo linapotokea wawe na uwezo wa kusaidia.

"Nitolee mfano tukio la ajali ya ndege ya abiria, raia walijitokeza kusaidia kuokoa jamii iliyokumbwa na ajali hiyo walikuwa wavuvi," alisema.

Waziri Mkuu alizindua nyaraka mbalimbali zikiwamo za mawasiliano ili kuwasiliana pale wanapokuwa wanafanya kazi.

Alifafanua kuwa serikali inafanya jitihada za kuweka utaratibu mzuri wa kushughulikia maafa, ikiwamo kutunga sera mbalimbali za kujenga.

Alisema sheria ya mwaka 2006 imebainisha vitu vyote kwa ajili ya maafa ambavyo ni vya msingi kwa jamii kuzuia na kupunguza majanga na kurejesha hali yanapotokea.

Alisema umeandaliwa mkakati wa maafa wa 2022 hadi 2027 na nyaraka hizo ni rafiki kwa sababu ziko za Kiswahili na Kiingereza.

Alisema mkakati unabainisha majukumu yaliyopo kwa lengo la kuimarisha uwezo wa nchi kupunguza maafa.

Alisema serikali iliona vyema kufanya mapitio na maboresho na yamezingatia kila kitu cha kuongeza katika mapitio ya vipengele mbalimbali vilivyoboreshwa.

Waziri Mkuu aliwataka kutenga fedha za maafa na watendaji wawe sehemu ya kuwajibika huku akitoa rai kwa Watanzania kuwa sehemu ya uwajibikaji na kuacha kulalamika.

Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Dk. Angelina Mabula, akimwakilisha Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu - Sera, Bunge na Uratibu, George Simbachawene aliwataka wananchi kuwa na tahadhari na mabadiliko tabianchi ili kuepuka maafa yatokanayo na mafuriko.



Askofu Mkuu wa kanisa la Evangelistic Assemblies of God Tanzania (EAGT), Dk. Brown Mwakipesile, akipanda mti kabla ya kuweka jiwe la msingi la ujenzi wa kanisa la EAGT Mwangaza, eneo la nyumba 300 Kisasa, jijini Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# DMI yapata dawa shida ya ajira

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KAIMU Mkuu wa Chuo cha Bahari Dar es Salaam (DMI) amewataka vijana kujiunga na chuo hicho ili kunufaika na fursa nyingi zilizopo ndani na nje ya nchi katika fani za ubaharia, hivyo kuukabili uhaba wa ajira uliopo nchini.

Dk. Tumaini Gurumo alibainisha hayo juzi jijini hapa alipotoa taarifa ya utekelezaji wa shughuli mbalimbali toka kuanzishwa kwake mwaka 1978.

Alisema vijana hawana budi kuchangamkia fursa zilizopo katika fani hiyo ya ubaharia kutokana na kuwapo mahitaji makubwa ndani na nje ya nchi.

"Hivi sasa kumekuwapo na malalamiko ya vijana kukosa ajira lakini katika fani hii mahitaji ni makubwa sana, hivyo vijana wetu hawana budi kujiunga na masomo haya ya ubaharia ili kukidhi mahitaji ya ndani na nje ya nchi," alisema.

Aliongeza kuwa chuo hicho hivi sasa kimejiimarisha tofauti na ilivyokuwa awali kilipokuwa na uwezo wa kutoa mafunzo katika ngazi za awali pekee.

"Hivi sasa chuo chetu ni chuo pekee nchini Tanzania na kimojawapo kati ya vyuo vya kikanda vinavyotoa mafunzo ya ubaharia kwa kuzingatia matakwa ya mkataba wa kimataifa unaosimamia elimu na mafunzo ya ubaharia na kinazingatia viwango vya ubora vya ISO 9000-2015," alisema.

Aliishauri serikali kuona umuhimu wa masomo ya ubaharia kuanza kutolewa kuanzia ngazi ya shule ya msingi ili kuwajengea uelewa wa masuala ya bahari Watanzania tangu wakiwa wadogo.

"Kutokana na nchi yetu kuzungukwa na bahari pamoja na maziwa, ipo haja serikali kuanza kutoa elimu ya masuala haya kwa watoto wa kuanzia shule ya msingi ili kuwapa uelewa wa masuala ya bahari hasa wakati huu ambao tunajikita katika kuimarisha uchumi wa bluu," alisema.

Pia alishukuru serikali kwa kukipatia chuo Sh. bilioni 6.5 ambazo wamezitumia kwa ajili ya kununua vifaa vya kisasa vya kufundishia.

"Vilevile, tunaishukuru serikali kwa kutupatia maeneo ambayo tunakwenda kujenga matawi ya chuo chetu na kusogeza huduma yetu karibu na jamii lakini pia kutokana na umuhimu wa fani hii, serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa ajili ya wanafunzi na katika mwaka huu wa masomo jumla ya wanafunzi 1,705 wamenufaika," alisema.

Aliyataja malengo ya chuo yanajumuisha kuanza kujenga vyombo vya usafiri wa bahari vidogo kupitia ujuzi walionao na kuviuza ili kuendelea kukuza uchumi wa bluu.

"Kujenga chuo katika ngazi ya juu ili kulingana na ukubwa wa jina tulionao na tunatarajia kujenga chuo hicho kikubwa katika ufukwe wa bahari Dar es Salaam na matawi yake yatakuwa mikoani," alisema.

Malengo mengine ni kuboresha karakana ili kuendana na mabadiliko ya kiteknolojia ili wahitimu wanapomaliza wasipate shida wanapoingia katika





## Bei ya petroli chini Zanzibar

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

BEI ya Mafuta ya Petroli Zanzibar imeshuka kwa mwezi Febuari kutoka Sh. 2,980 bei ya Januari hadi kufikia S.h 2,880.

Akizungumza jana na waandishi wa habari ofisini kwake Maisara mjini Zanzibar, Kaimu Meneja Uhusiano wa Mamlaka ya Udhibiti wa Maji na Nishati Zanzibar (ZURA), Shara Chande, alisema mamlaka hiyo hupanga bei kwa kuzingatia wastani wa mwenendo wa mabadiliko wa bei za mafuta duniani.

Alisema pia wanaangalia gharama za uingizaji wa mafuta katika Bandari ya Dar es salaamu na Tanga, thamani ya shilingi ya Tanzania kwa dola za kimarekeani na kodi na tozo za serikali.

Pia alisema mamlaka huangalia gharama za usafiri, bima na bei halisi ya mafuta (premium) hadi Zanzibar na kiwango cha faida kwa wauzaji wa jumla na rejareja.

Kaimu meneja huyo alisema kwa bei ya mafuta ya dizeli, ya taa na ya ndege, bei haijashuka na ipo kama ilivyotumika Januari.

"Bei ya mafuta ya dizeli ni 2,990, mafuta ya taa ni 2,921 na mafuta ya ndege ni 2,681," alisema.

Hata hivyo, alisema mamlaka hiyo inaendelea na kufuatilia na kudhibiti soko la mafuta na bei zake kwa ukaribu ikiwa ni pamoja na kuhakikisha bei za bidhaa hizo haziongezeki na kutoleta athari katika shughuli za kijamii na kiuchumi.

Aliwataka wananchi kununua mafuta katika vituo halali vya mafuta na kudai risiti za kielektroniki kila wanaponunua mafuta.



Mratibu wa mradi wa kuimarisha kilimo cha mboga wa shirika la kimataifa la utafiti, uendelezaji na uhamasishaji wa mazao ya mboga, Jerimah Sigalla (kulia), akiwasilisha malengo ya mradi huo, kwa wadau mbalimbali, katika ofisi za Wizara ya Kilimo Zanzibar Maruhubi jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# WVC yabainisha soko kubwa la mboga

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI wa Shirika la Kimataifa la Utafiti, Uendelezaji na Uhamasishaji wa Mazao ya Mboga (WVC), Dk. Gabriel Rugalema, amesema Zanzibar ina soko kubwa la mboga kwa sababu ina hoteli nyingi za kitalii.

Amesema hoteli zilizopo visiwani hapa ni 672 na kati ya hizo, 500 zina hadhi ya nyota tano lakini asilimia 66 ya vyakula vinavyoliwa hotelini zikiwamo mboga vinatoka nje ya Zanzibar.

Dk. Rugalema aliyasema hayo jana katika kikao maalum cha kutambulisha mradi wa kuimarisha kilimo cha mboga walengwa wakuu wa mradi huo wakiwa vijana na wanawake.

"Tunaweza kuzungumza na wamiliki wa hoteli hizo za kitalii kuagiza mboga na matunda hapa hapa Zanzibar ili kuongeza ajira nyingi kwa vijana. Asilimia 33 ya vijana wa Zanzibar hawana ajira inayotambulika rasmi," alisema.

Lengo la mradi huo, alisema ni kuongeza ajira, kubadilisha hali ya upatikanaji wa mboga kuwa bora, kuimarisha lishe bora huku akibainisha kwamba mboga za majani za kiafrika zinasaidia sana katika kuongeza lishe bora na kuleta mabadiliko katika jamii.

Alisema lazima Zanzibar ifanye utafiti kuangalia afya ya udongo kwa sababu utafiti wa udongo umefanyika miaka mingi tokea miaka ya 1990 na udogo ni kiumbe hai kinachobadilika kama binadamu. "Udongo unabadilika afya yake, hivyo ni vyema kuangalia afya ya udongo kufanya utafiti na kuleta ramani mpya. Watunga sera wataziangalia na kusema udongo gani unafaa kwa matumizi gani, udongo gani kwa ujenzi na udogo gani utunzwe kwa kilimo" alisema.

Dk. Rugalema alisema udongo ukiwa wa kilimo lazima kuwa na mbegu bora lakini Zanzibar inategemea mbegu kutoka kampuni za mbegu ya Tanzania Bara, hivyo kuna mwanya wa kuwa na mbegu bora na kwamba mradi huo pia utajikita uzalishaji wa mbegu visiwani humo.

"Mbegu bora ndio ustawi wa wakulima na bila ya mbegu bora huwezi kuzalisha hata ukiwa na udongo mzuri," alisema Dk. Rugalema.

Alisema mradi pia unaangazia mazingira ya biashara katika kilimo cha mboga na matunda kwa vijana na wanawake na kuongeza thamani ya mazao hayo.

Akifungua kikao hicho, Mkurugenzi wa Sera na Utafiti kutoka Wizara ya Kilimo, Malialisi, Umwagiliaji na Mifugo, Sihaba Haji Vuai, alisema wizara inaelekea katika kuifanyia mabadiliko Sera ya Kilimo ya mwaka 2010 kutokana na changamoto mbalimbali zilizopo katika sekta ya kilimo.

Sihaba alisema changamoto kubwa iliyoko katika kilimo kuwapo kwa uvamizi katika ardhi kilimo kutokana na kasi ya ujenzi wa nyumba za makazi kwa sababu ya ongezeko la idadi ya watu.

Alisema ili kudhibiti hali hiyo, ni vyema kupunguza matumizi ya ardhi kwa kujenga nyumba za gorofa kwa ajili ya makazi ambazo zitachukua eneo dogo la ardhi na wananchi wingi kupata makazi.

Eneo dogo la ardhi lilolopo, alisema linahitaji utalamu mkubwa ili kuzalisha mazao mbalimbali na wananchi wingi kufaidi na mazao yaliyopo.

Akiwasilisha mada kuhusu malengo ya mradi huo, Mratibu wa Mradi huo, Jeremiah Sigalla kutoka Shirika la Kimataifa la Utafiti, Uendelezaji na Uhamasishaji wa Mazao ya Mboga, alisema wafaidika wakubwa wa mradi huo ni wanawake na vijana kwa sababu ndio wanaokumbana na changamoto ya ukosefu wa ajira.

# Wataka mabadiliko sheria kandamizi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WADAU wa habari Zanzibar wamesema kuna haja ya kufanyia marekebisho sheria ambazo zinakinzana na upatikanaji wa habari na uhuru wa vyombo vya habari ili kuchochea uwajibikaji na upatikanaji wa taarifa kwa lengo la kuleta maendeleo katika jamii.

Mmoja wa wadau hao, Jabir Idrissa, alisema suala la upatikanaji wa habari na uhuru wa habari si suala linalolenga kuwanufaisha waandishi na vyombo vya habari pekee bali ni suala mtambuka lenye manufaa ya kujenga uwajibikaji kwa viongozi na jamii.

Aliyasema hayo jana wakati wa mafunzo kwa waandishi wa habari ya kuwajengea uwezo kutambua upungufu uliomo katika sheria za habari na kujadili mkakati wa kufanya uchechemuzi wa mabadiliko ya sheria hizo ili kuweka mazingira rafiki ya vyombo vya habari Zanzibar.

Jabir alisema kuwapo sheria zinazotoa fursa kwa vyombo vya habari kutekeleza wajibu wao kwa uhuru bila vikwazo vya kisheria, kunatoa nafasi kwa waandishi wa habari kusaidia jamii na mamlaka kuibua changamoto zilizopo katika maeneo mbalimbali na kutatuliwa kwa wakati. Alitaja miongoni mwa sheria ambazo zimebainika kuwa na upungufu unaohitaji kufanyiwa marekebisho ni Sheria ya Usajili wa Wakala wa Habari, Magazeti na Vitabu Na. 5 ya mwaka 1988 iliyofanyiwa marekebisho na sheria Na.8 ya mwaka 1997, Sheria ya Tume ya Utangazaji ya Zanzibar Na. 7 ya mwaka 1997 kama ilivyorekebishwa na sheria namba 1 ya mwaka 2010 pamoja na Sheria ya Makosa ya Mtandao ya mwaka 2015.

Zingine ni Sheria ya Kufuta Sheria ya Baraza la Wawakilishi (kinga, uwezo na fursa) namba. 4 ya 2007 na kutunga sheria mpya ya Baraza la Wawakilishi (kinga, uwezo na fursa) katika kutekeleza kazi na mambo mengine yanayohusiana na hayo Na. 6 ya 2022, Sheria ya Kufuta Sheria ya Uchaguzi namba. 11 ya 1984 na kutunga Sheria ya Uchaguzi ya mwaka 2017 na masuala mengine yanayohusiana nayo.

Akiwasilisha mapitio ya Sheria ya Usajili wa Wakala wa Habari, Magazeti na Vitabu Na. 5 ya mwaka 1988 iliyofanyiwa marekebisho na sheria Na. 8 ya mwaka 1997, Imane Duwe, mkufunzi wa habari kutoka Chuo Kikuu cha Taifa Zanzibar (SUZA), alisema Kifungu cha 3 cha sheria hiyo kimempa Waziri mamlaka ya kuteua Msajili wa Vitabu na Magazeti lakini iko kimya juu ya sifa na uzoefu wa msajili huyo.

"Nafasi ya msajili inatakiwa itangazwe na apatikane kwa mujibu wa sifa, mfano awe mwanasheria au mtu mwenye taaluma ya habari na mawasiliano ya umma na sifa za msajili zinapaswa kuainishwa katika sheria," alisema.

Pia alisema kuhusu upatikanaji wa taarifa, hakuna kifungu kinachozungumzia haki ya muandishi wa habari kupata taarifa kutoka kwa mamlaka mbalimbali.

Mkurugenzi wa Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) Zanzibar, Dk. Mzuri Issa, aliwataka waandishi wa habari kuendelea kufanya ushawishi wa mabadiliko ya sheria zenye upungufu ili kutoa fursa ya upatikanaji wa sheria zinazoweka mazingira bora kwa vyombo vya habari Zanzibar kutekeleza majukumu yao. "Haki haiji mezani. Ni lazima tukazane, tusiogope sheria na wala tusikate tama. Tuendelee kuandika kwani sheria zipo kwa ajili yetu ili mradi tunachokifanya ni kitu sahihi hatuvunji sheria. Twende tukaandike zaidi kwani tunafanya uchechemuzi ili wananchi wapate taarifa zinazowaletea maendeleo," alisema.

Salim Said Salim, mwandishi wa habari mwandamiz, aliwataka waandishi wa habari kuzungumzia kifungu baada ya kifungu badala ya kuangalia upungufu wa sheria kandamizi kwa uhuru wa habari ili kusaidia kufanikisha lengo la uchechemuzi wa mabadiliko ya sheria hizo.

"Sisi waandishi wa habari tunao wajibu mkubwa wa kuwafahamisha viongozi na wananchi wote kwamba tunapozungumzia uhuru wa habari si kwa manufaa ya waandishi na vyombo vya habari tu bali ni kwa manufaa ya jamii nzima kupata huduma zao muhimu," alisema.

Mafunzo hayo yaliandaliwa na TAMWA Zanzibar kupitia Shirika la Internews Tanzania kwa kushirikiana na wadau wingine wa habari Zanzibar kuangalia upungufu uliomo katika sheria zinazosimamia sekta ya habari Zanzibar.



## BRITNEY SPEARS
UKURASA 14



# MTOTO MKAIDI HAFAIDI



SASA mwanamuziki wa Bongo Fleva, Harmonize, amejikuta akizungumza peke yake, anajilaumu na kujiona hana maana katika jamii.

Kulingana na kile anachopitia, inaonekana kila anachokifanya kwa sasa hakiwezi kumpatia furaha ambayo ameipoteza baada ya kutendwa.

Tangu kuachana na aliyekuwa mpenzi wake Kajala Masanja, ambaye ni mwigizaji wa Bongo Muvi, hajakaa sawa na kila anachokisikia kutoka kwa watu wanaomzunguka au nje ya hapo, inamjengea hasira na kujilaumu.

Hivi karibuni, Harmonize kupitia mtandao wa Instagram, amebainisha mbele ya watu nini kinamsumbua moyoni mwake na kusababisha kuwa na migogoro mingi ya nafsi.

Kwenye ujumbe wake, Harmonize amekiri kwamba aliyekuwa mwanamke ambaye anampenda sana ilibaki hatua chache azifikie ili afunge naye ndoa, lakini hali ilibadilika na kuwa majuto.

Bila ya kumtaja jina lake, mwanamuziki huyo ameeleza kwa mtindo wa kuonya jinsi mapito yake yalivyokuwa, huku mama yake akijaribu kumshauri lakini hakufua dafu.

Katika ujumbe wake huo ambao unawaonya vijana kukubali ushauri kutoka kwa wazazi, inaonyesha Harmonize wakati penzi lake likistawi, kuna wakati alionywa lakini aliona kama vile anaonewa.

Harmonize ameendelea kuonyesha sononeko lake kwa kuwataka vijana chochote watakachosema wazazi au walezi wasikilizwe sana kwani yana maana ndani yake.


Kwa kuwa yeye alikengeuka na kutoyasikia ya mkuu, basi ameelezea kwa masikitiko kwamba wazazi wanaona mbali, hasa kama kuna kitu unafanya ambacho hakipo sahihi.Kwa ujumla mwanamuziki huyo anatambua kwamba kila penye mafanikio hapa duniani inatokana na radhi ya wazazi, na endapo ukiwa mkaidi unaweza kutofika safari.

BASI SAWA

## Harmonize bachela boy

Msanii Harmonize baada ya kusema kwa sasa hayupo kwenye mahusiano ya kimapenzi na mwanamke yoyote, ameamua kuweka bango kabisa kusisitiza kuwa hajaona, hana mpenzi yoyote na yupo peke yake.

Msanii huyo ambaye hadi mwaka jana alikuwa na uhusiano ya msanii wa filamu, Kajala kabla ya kumwagana, mara kwa mara amekuwa akisisitiza kuwa hana mpenzi na kwa sasa hatarajii kuwa naye hivi karibuni.



Kuna dada mmoja aliamua kuchora tatoo yake, kwa mapenzi ya ushabiki au kutaka kuwa naye kwenye mahusiano, lakini hata baada ya Hamronize kusikia na kuliona hilo, akamjibu kuwa anashukuru lakini hataki kabisa kuingia kwenye mahusiano kabisa.

Kama vile haitoshi, labda baada ya kuona kama vile hawamsikii, akaamua kuweka bango kubwa pale sehemu za Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam kusisitiza kile alichokibainisha.

## Udaktari wa Babu Tale siyo wa vidonda

Mbunge wa Morogoro Kusini Hamisi Shaban Taletale, maarufu kama Babu Tale, wamewaambia wale ambao kama wana nongwa hivi na udaktari wake siyo ule wa kufanyia watu operesheni au kushika vidonda, bali ni wa heshima kutokana na kile ambacho amekifanya kwenye jamii.



Babu Tale ambaye ni meneja wa msanii maarufu Afrika kwa sasa, Diamond Platnumz amesema kuwa hata baadhi ya wabunge wenzake wanadhani labda amepewa kwa sababu ya ubunge na kukaa bungeni kwa miaka miwili

"Wengi hawakuelewa udaktari wangu, sijapata udaktari wangu kwa ajili ya kukaa bungeni miaka miwili, nimepata udaktari wa heshima wa kile nilichokifanya kwenye fani yangu na kwenye jamii inaonekana.



## ANJELA ASEMA HANA MANENO MENGI

Msanii Anjela ambaye anayejitegemea baada ya kuondoka kwenye lebo ya Konde Gang amewataka wasanii kufanya kazi na siyo kuwa na maneno mengi.

Msanii huyo amesema msanii kujulikna, kuthaminika na kuheshika kutokana na kazi zake anazozifanya na si maneno.

"Kitu ambacho nawaasa wasanii ni kutokuwa na maneno mengi, kazi ndiyo izungumze na si wao, kwa sababu mashabiki wanangalia zile nyimbo zao na ubunifu wao na wala siyo kuongea sana kwani siyo ambacho mashabiki wanahitaji kutoka kwao," alisema. Anjela alitamba akiwa na Harmonize kwa ngoma kama 'Kioo', 'All Night', 'Kama', 'Toroka', 'Nobody', 'What Do You Miss' na nyingine nyingi.





## Jux mapenzi na kazi baba

Msanii Jux amesema mapenzi hayawezi kumzuia yeye kutofanya kazi zake kisanii au kumrudisha nyuma, sana sana zinamfanya afanye vema zaidi.

Jux alisema katika maisha yake tangu aanze mambo ya mahusiano, hajawahi kukaa 'singo' kwa muda mrefu na amekuwa akifanya vizuri sana kwenye tasnia ya muziki.

"Kusema mapenzi yanazuia usifanye kazi vizuri, kwangu hiyo haiwezekani, mimi ni mara chache sana huwa niko 'singo', siwezi kukaa muda mrefu bila mahusiano.

Nitakaa na mtu, tutagombana, nitaachana naye, baada ya muda nitapata mwingine, nimeshazoea kuwa hivyo. Sidhani kama imeshawahi kuniathiri. Hata albamu hii mpya wakati nafanya, huyu msichana wangu nilikuwa naye kiasi cha miaka miwili nyuma, na bahati nzuri ninapokuwa na mtu, napenda kwanza ajue kazi yangu na asili ya kazi hiyo na ugumu wake kwa hiyo sidhani kama mapenzi yanaweza kunirudisha nyuma kimuziki."

## DUNIA NI HII HII WAPITAYO VIUMBE

**Na Adam Fungamwango**

UKISIKILIZA hadithi nyingi na mambo mengi ya zamani na hata ukisoma kwenye vitabu mbalimbali vyenye kuheshimika, utagundua hakuna kitu kipya hapa duniani kinachofanyika.

Yote ni yale yale tu. Ni kama vile wanasayansi wanavyosema dunia inajizungusha yenyewe kwenye mhimili wake na kweli yote yanayofanyika yanajirudia tu.

Tena kuna vitu vingine vilifanyika zamani hadi leo hii havijafanyika tena. Vinavyoendelea kujirudia ni baadhi ya mambo machache tu yaliyofanyika miaka milioni nyingi huko nyuma.

Ndiyo maana utasikia watu wanakwambia maisha ya sasa ni magumu. Lakini ukisikia nyimbo za miaka 50 nyuma, utakuta wanaimba maisha ya sasa ni magumu. Ina maana yalianza kuwa magumu tangu zamani. Hivi sasa kuna udanganyifu wa mapenzi. Ukisoma vitabu vya miaka mingi nyuma, utakuta pia kulikuwa na udanganyifu.

Leo katika mada hii tutaziangalia nyimbo ambazo zinazungumzia dunia, raha, matatizo yake na vituko zilizotungwa miaka ya 1980 mwanzoni hadi mwishoni.

**Dunia Duara-Shaaban Dede**

Shaaban Dede akiwa na Bima Lee, alitunga kibao cha 'Dunia Duara'. Hiki kinazungumzia juu ya mtu anayechekwa na wenzake kuwa hana kitu.

Lakini mwenyewe anajipa matumaini kuwa dunia ni duara na huzunguka, hivyo anajua kesho atapata kwa jinsi anavyojituma. Anasema jua halina mpaka, huangaza pote kwa hiyo ipo siku na yeye ataangaziwa, kwani kama samaki baharini, wadudu mapangoni na wanyama porini wanaishi, basi kwa kudra za Mungu na yeye atapata tu.

**Dunia Uwanja wa Fujo-Marijani**

Jabali la Muziki Marijani Rajab, yeye akatunga kibao cha 'Dunia Uwanja wa Fujo'. Anawatahadharisha wote wanaojimwambafai na kuiona dunia kama yao, kuwa walikuwepo watemi, wafalme wenye nguvu, lakini leo hii hawapo.

Alikuwepo Firauni, Hitler, Nduli Idd Amini ambao historia inasema ni moja kati ya viongozi wababe kuwahi kutokea duniani, lakini kwenye dunia hii hakuna mbabe kushinda Mwenyezi Mungu.

Kwa maana hiyo anawaasa watu hususan wanaopewa dhamana, kuishi vizuri na watu, kwa sababu ubabe hauna maana akamalizia kwa kusema kwenye dunia hii 'kula ugali wako ukalale'.

**Dunia-Remmy Ongalla**

Remmy Ongalla kwenye fasihi yake ya wimbo huu wa 'Dunia' anasema yote ambayo binadamu atakayofanya hapa duniani, ikiwa ubaya au wema, atalipwa hapa hapa ulimwenguni.

Anasema kwa Mungu hatupajui, hivyo binadamu anatakiwa kutenda wema, kwani kuna baadhi ya watu hudhulumu wengine kwa vyeo vyao, wadhifa, pesa na umaarufu.

**Dunia-TX Moshi William**

Akiwa na bendi ya Polisi Jazz, kabla ya kujiunga bendi ya Juwata Jazz, alitunga kibao kisemacho 'Dunia'. Anauliza, mwezi na nyota usiku zinang'aa bili yake analipa nani? Na ilitakiwa kabisa aulizwe anayelipwa bili ni nani? Huyo ni mwenyezi Mungu. Yeye kila kitu hutoa bure kwa waja wake.

**Dunia Imani Imekwisha-Marijani**

Hapa Marijani amerudi tena hapa na wimbo wa 'Dunia Imani Imekwisha'. Yoyote aliyedhani eti sasa ndiyo kuna dhana hiyo, lakini hata miaka ya 1970 hadi 1980, kulikuwa na matendo kiasi cha kuonekana dunia imani yake ni ndogo.

Watu wanaibiana. Wanatapeliana. Wanadhulumiana. Kuna wanaodhulumu watoto yatima. Wanaotaka kuwaua wazazi wao ili warithi mali na mengine mengi.

FILAMU

# Mtoto wa Kambo: Tabia ya mtu haibadiliki

**Na Adam Fungamwango**

WASWAHILI wanasema tabia ya mtu haibadiliki, ni kama ngozi ya kwapa hata huisafishe vipi, itabaki vile vile tu.

Imekuwa ni kama kasumba kama si Afrika bali dunia nzima kuwahusisha mama wa kambo na ubaya, ukatili na unyanyasaji.

Linapokuja neno mama wa kambo, basi moja kwa moja kichwani inakujia taswira kuwa ni mtu mbaya, ambaye kazi yake ni kutowatendea haki watoto wa mumewe aliyewakuta.

Hata hivyo wakati mwingine huwa si kweli. Ni kwa sababu tu watu wamekariri. Wakati mwingine kuna watoto wa kambo nao ni tatizo, lakini hili mara nyingi halisemwi.

Kwa maana hiyo, roho mbaya, ukatili na unyanyasaji ni tabia ya mtu tu na wala si mama wa kambo tu, bali kuna hata baba wa kambo na watoto wa kambo wenye tania hiyo.

Hilo linathibitishwa kwenye filamu inayoitwa 'Mtoto wa Kambo' iliyochezwa na kina Princess Salha kama mama Zubeda, Hatma Omari yeye alicheza kama Siwa, Mwajabu Madiwa aliigiza kama Doido, Ireen Chacha alicheza kama Zubeda, Omary Mtango ni Mzee Aman, mzee Marimba yeye alicheza kama Marimba.

Mzee Aman anaishi na mke ambaye alimuona baada ya mke wake wa kwanza kufariki dunia. Marehemu alimuachia mtoto mmoja wa kike, Doido na mke aliyenaye amemzaliwa binti aitwaye, Zubeda.

Awali waliishi vizuri tu, lakini ghafla Doido alianza kubadilika kitabia. Akaanza kumnyanyasa mdogo wake Zubeda akiwambia pale si kwao, akimpiga na kumfanyia kila aina ya vituko yeye na mama yake.

Kuna siku alijikata mwenyewe makusudi na kumsingizia mdogo wake. Mzee Aman aliamini hivyo na kumpiga Zubeda. Mzee aliona kama binti yake Doido ananyanyaswa kwa sababu mama yake amefariki, lakini ukweli ni kwamba Doido ndiye alikuwa akiwanyanyasa mdogo wake na mama yake wa kambo.

Siku moja anamweleza waziwazi mdogo wake kuwa anamchukia sasa yeye na mama yake, hivyo anawatafutia sababu ili waondke pale kwani amepata mchumba anataka kuishi naye pale kwa baba yake.

Na kweli anafanya hivyo kwa kumueleza baba yake kuwa mama ana mpango wa kumuwekea sumu kwenye chakula na amewasikia mwenyewe kwa sauti yake.

Kwa hasira mzee Aman anamtimua mkewe na binti yake Zubeda ambao wanakimbiliwa kwa mjumbe mzee Marimba.

Mzee huyo katika kusuluhisha anamwambia Aman kuwa awe anachunguza mambo na si kusikiliza upande mmoja.

Zubeda na mama yake wanarejea kuishi tena hapo nyumbani, lakini wakiwa kama wafungwa.

Za mwizi arobaini, kwani Zubeda aliamua kumueleza baba yake mzazi sababu ya yale yote yanayotokea nyumbani hapo, ikiwemo Doido kutaka wasikae pale.

Siku chache tu baadaye Doido anamwita mdogo wake na kuanza kumchamba kwa kwenda kumueleza baba yake mambo yake.

"Kama unaona donge kuwa na mchumba na wewe tafuta wa kwako." Yalikuwa ni baadhi ya maneno aliyoyasema ambayo yalinasawa vema na mzee Aman na kuthibitisha kuwa ni kweli mbaya anayeiyumbisha familia ni binti yake Doido mtoto wa marehemu mkewe. Mambo yamegeuka, alikwenda kumtia makofi Doido na bakora juu.



# Britney basi tena

IMEELEZWA hali ya mwanamuziki, Britney Spears, imezidi kuwa mbaya kutokana na kuongezeka kwa matatizo ya afya ya akili na matumizi makubwa ya dawa za kulevya.

Imeelezwa familia yake na watu wa karibu wanapanga kuingilia kati kutokana na afya yake kuzidi kuzorota tangu apewa mamlaka ya kuhodhi mapato yake.

Kulingana na mtandao wa TMZ, kilimtunuku mtu mmoja wa karibu na msanii huyo ambaye amesema anahofia anaweza kufa muda si mrefu.

Watu karibu na Britney wamefadhaishwa na tabia yake isiyobadilika.

"Tunaambiwa anachukua dawa kwa wingi na anazitumia," kilisema chanzo kingine.



## Bucharach afariki dunia

MTUNZI mahiri wa nyimbo katika historia ya Marekani, Burt Bacharach, amefariki dunia juzi.

Bacharach alihusika na vibao vingi vya wanamuziki nyota kama vile "Raindrops Keep Fallin' on My Head" na "I Say a Little Prayer"

Taarifa zinaeleza alifariki katika hospitali yake ya L.A. kwa sababu za uzee.

Bacharach ambaye alimuandikia nyimbo Hal David, na kusifika na nyimbo kama "Do You Know The Way to San Jose," "Walk on By," "I'll never Fall in Love Again" na "Don.

Wanamuziki wengine walionufaika na utunzi wake ni Aretha Franklin, Elvis, Dusty Springfield, Frank Sinatra na Tom Jones.

## Kuti, Peter wachambuana

Uchaguzi wa Nigeria unapozidi kukaribia, baadhi ya wasanii wamejikuta wakikabiliana wao kwa wao kutokana na kuwa na mitazamo tofauti.

wanamuziki wawili Seun Kuti na Peter Okoye, wamejikuta wakitupiana vijembe kwenye mitandao ya kijamii kwa kila mmoja akimtuhumu mwenzake kuunga mkono chama ambacho anaamini hakina malengo.

Suala lilianza pale Kuti aliposema anaamini kuwa hakuna mwanasiasa anayeweza kuokoa Nigeria isipokuwa Wanigeria wenyewe.

Akijibu hilo Okoye amempinga kwa kusema ni jambo la aibu kusikia mtu akisema hakuna mgombea ambaye anaweza kuiokoa nchi hiyo.





## Funke amlilia mama yake

MWIGIZAJI mkongwe na mtayarishaji wa filamu za Nollywood, Funke Akindele, amepata pigo baada ya kumpoteza mama yake mzazi ambaye amefariki dunia wiki hii.

Taarifa iliyotolewa na dada yake Funke, Olubunmi Akindele, ilisema familia imekuwa na mioyo mizito na majonzi kwa kumpoteza mama, dada na bibi.

"Familia ya Adebanjo na Akidele inatangaza kuondokewa na binti yao, mama na dada, Dk. R B Adebanjo-Akindele, kilichotokea Jumanne," ilisema taarifa hiyo.

## Portable azidi utata

MWIMBAJI mwenye utata kutoka Nigeria, Habeeb Okikiola, maarufu kama Portable, amefichua kwamba huwa anavutana na watu kwenye mitandao ya kijamii ili kujilinda.

Portable amesema katika mahojiano na Timi Agbaje, kwamba mabishano kwenye mitandao yanamuweka salama na watu ambao huwa wanamvuruga.

Amesema kuwa watu huwa wanamshambulia kutokana na jinsi anavyoishi na ili awe salama ni muhimu kuwafuata huko na kubishana kwa hoja.





## RC aagiza halmashauri kutenga fedha kwa ajili ya lishe shuleni

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MKUU wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, ameagiza Wakurugenzi wa Halmashauri za mkoa huo, kuhakikisha mnatenga na kutoa Sh. 1,000 kwa kila mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano ili kusaidia utekelezaji wa mpango wa afua za lishe na udhibiti wa udumavu kwa watoto.

Makongoro aliagiza hayo jana wakati wa kikao kazi cha utekelezaji wa mkataba wa lishe kwa kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka jana.

"Wakurugenzi wote mnatakiwa kutoa Sh. 1,000 kwa kila mtoto ili zisaidie afua za lishe," aliagiza Makongoro.

Alisema ili mkoa uweze kufikia malengo yake, idara ya afya inatakiwa kuimarisha tiba, kuimarisha huduma za lishe, kuimarisha huduma za wajawazito na watoto na kusimamia ubora wa lishe.

Alisema fedha zote zilizotengwa kwa ajili ya afua za lishe, zitumike mpaka Juni mwaka huu na apate taarifa.

"Suala la lishe ni muhimu sana, unaweza ukakuta mtoto ni mtulivu na hakosi darasani ila kumbe amedumaa na ambaye ni mtukutu anafanya vizuri darasani kumbe hajadumaa," alifafanua. Awali Ofisa Lishe wa Mkoa wa Manyara, January Dalushi, akizungumza katika kikao hicho, alisema kwa mujibu wa utafiti wa kitaifa uliofanyika mwaka 2018, udumavu kwenye Mkoa wa Manyara uko asilimia 36.1. Ofisa Lishe huyo alisema halmashauri nyingine hazijafikia kiwango kinachopangwa kutolewa cha Sh. 1,000 kwa mtoto mmoja.

Dalushi alisema ili kutekeleza vizuri mkataba huo wa lishe, wanapaswa kupanga bajeti ya lishe kwenye vyanzo vya fedha vyenye uhakika kwa mwaka wa fedha 2023/24.

Akichangia mjadala huo wa lishe, Ofisa Mipango na Uratibu wa Mkoa huo, Maarufu Mkwaya aliwaomba wakurugenzi kutenga fedha Sh. 1000 kwa watoto na wanapozitenga waangalie wanazipeleka wapi.

PKatibu Tawala Msaidizi Sekretarieti ya Mkoa anayeshughulikia afya, Dk. Damas Kayera alisema hawatapitisha bajeti ya lishe kama halmashauri hazitazingatia maelekezo ya serikali.

Dk. Kayera alisema hivi karibuni watafanya tathmini ya lishe ili kubaini udumavu kwa mkoa huo kama umepungua kwa kuwa wanatumia takwimu za nyuma.

Ofisa Lishe wa Halmashauri ya Mji wa Mbulu, Adam Mhako alisema wana uhaba wa vitendea kazi katika vipimo na hawana kipimo cha ukondefu kwa watoto.

Mhako alisema kwa kipindi cha Julai hadi Desemba mwaka jana, waliwapatia nyongeza ya matone ya vitamin A watoto 29,209.

# Shule zisizokuwa na vyoo zakumbukwa

**Na Godfrey Mushi,** HAI

HATIMAYE serikali imeanza kutafuta suluhu ya kudumu ya tatizo la ukosefu wa vyoo kwenye shule zake tisa za msingi za Usari, Narumu, Marire, Chekereni, Msamadi, Kambi ya Raha, Uswaa, Waramu na Mbatakero zilizoko Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro baada ya kuzitengea zaidi ya Sh. milioni 118.8 kwa ajili ya kufuta aibu hiyo.

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya hiyo, Dionis Myinga alisema jana kuwa katika Shule ya Msingi Usari, serikali inakusudia kujenga matundu ya vyoo 12, Narumu (12), Marire (12), Chekereni (12), Msamadi (12), Kambi ya Raha (12), Uswaa (12), Waramu (12) na Mbatakero (12), sawa na jumla ya matundu ya vyoo 108.

Alikuwa akizungumza jana katika mkutano wa Baraza Maalum la Madiwani lililoketi kwa ajili ya kupitisha mapendekezo ya mpango na bajeti ya halmashauri hiyo kwa mwaka wa fedha 2023/24, inayotarajiwa kutumia zaidi ya Sh. bilioni 43,365,519,984 na maombi maalum ya Sh. 16,996,00.

Wakati anawasilisha makisio ya miradi na shughuli za maendeleo zitakazotekelezwa kwa fedha za mapato ya ndani (asilimia 40), kwa mwaka wa fedha ujao, Myinga alisema serikali pia inatarajia kukamilisha ujenzi wa matundu ya vyoo vya wanafunzi kwenye shule nne za msingi Orori, Shirimatunda, Machame na Narumu Tella kufikia Juni mwakani.

"Lakini sio hayo tu, kuna Shule 10 za Msingi za Narumu, Usari, Orori, Kingereka, Waramu, Uswaa, Miaseni, Mlima Shabaha, Kambi ya Raha na Nsongoro zimetengewa Sh. 558,240,000, zitatekeleza miradi ya madarasa ya mfano ya awali 20 na matundu ya vyoo vya wanafunzi wa awali 60 kupitia programu maalum ya Lipa Kulingana na Matokeo.

Mkurugenzi huyo alisema halmashauri hiyo pia inakusudia kujenga matundu 53 ya vyoo kwenye Shule za Sekondari za Hai Day 20, Boma (20), Tumona (10) na Sekondari ya Kyuu (7) ifikapo Juni mwaka 2024.

Desemba 5 mwaka jana, Nipashe iliripoti kuhusu walimu na wanafunzi wa shule hizo kutumia choo kimoja na wanafunzi, huku ikielezwa kuwa watawa wa Kanisa Katoliki, Parokia ya Narumu, wamekuwa wakiwasitiri walimu wa Shule za Msingi Usari na Narumu kupata huduma ya choo.

Katika kikao hicho, Mwenyekiti wa Halmashauri hiyo, Edmund Rutaraka aliagiza mkurugenzi huyo kuwasukuma watendaji wa idara ya mapato kuhakikisha wanapeleka mashine za kielektroniki za kukusanyia mapato (POS) kwenye masoko mapya ya Maiputa na Gezaulole ili kuisaidia halmashauri hiyo kufikia malengo yake ya kukusanya mapato.



Mwongoza watalii mlimani kutoka kampuni ya Utalii ya ZARA Tours, Bruce Temba (katikati), akifafanua jambo kwa watalii, mjini Moshi jana kabla ya kuanza safari yao ya siku sita ya kupanda Mlima Kilimanjaro hadi kilele cha juu kabisa cha Uhuru (5,895m ASL), kupitia njia ya Marangu. **PICHA: JAMES LANKA**

# Mkulima anaswa na makachero kwa tuhuma za kulima bangi

**Na Steven William,** MUHEZA

MAKACHERO wa Jeshi la Polisi mkoani Tanga, wanamshikilia mkulima Elia Kunguru, mkazi wa Kijiji cha Mwarimba, Kata ya Misozwe, Wilaya ya Muheza, kwa tuhuma za kulima na kumiliki shamba linalodaiwa kuzalisha dawa za kulevya aina ya bangi.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Upelelezi wa Wilaya hiyo, Charles Ntenga, mtuhumiwa huyo alikamatwa jana baada ya kufanyika operesheni ya kushtukiza kwenye kijiji hicho.

"Ni kweli tunamshikilia lakini bado hatujafahamu bangi iliyokuwa kwenye shamba hilo ni kiasi gani. Tumeikuta bangi hiyo ikiwa bado mbichi na imeoteshwa katika shamba la mkulima huyo. Tunaendelea na uchunguzi zaidi ili kujua mtandao wa wakulima wengine wa dawa hiyo.

"Operesheni hii inahusisha Wenyeviti wa Serikali za Vijiji na katika Kijiji cha Mwarimba tulimshirikisha Mwenyekiti wake, Rogers Kanju kufika eneo la tukio, kukamata mhusika na kupanga kazi ya kuharibu mazao hayo," alisema.

Aliongeza kuwa Jeshi la Polisi lilipata taarifa kutoka kwa watu wema kwamba kuna mkulima analima bangi kwenye kijiji hicho na ndipo walipoamua kumfuatilia na kugundua ni kweli.

Akizungumzia tukio hilo, Mwenyekiti wa Kijiji cha Mwarimba, Rogers Kanju alisema kitendo cha wanakijiji wake kulima bangi na kuvuta kinamkera kama kiongozi na ndio maana ameamua kutoa ushirikiano kwa vyombo vinavyousika ili kukomesha ulimaji wa zao hilo. Alidai alikuwa hafahamu kwamba kwenye kijiji chake kina mkulima analima bangi, hivyo analishukuru Jeshi la Polisi kwa kugundua hilo huku akisema hana ushirikiano kabisa na wakulima wa bangi kwenye kijiji hicho na polisi watambue hilo.

Mwezi Mei mwaka jana, Kamishna Jenerali wa Mamlaka ya Kudhibiti na Kupambana na Dawa za Kulevya (DCEA), Gerald Kusaya alinukuliwa na Nipashe akisema mashamba yatakayobainika kulima bangi na mirungi, kuanzia sasa yatataifishwa kwa manufaa ya umma ili kukomesha biashara hiyo.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA...

# Watoto walivyokuwa 'wanamaindi' baba kula paja, nyama kubwa, kidari

## -Ukikosa nyama, unakwenda uani kwa mama kuangua kilio



Na Adam Fungamwango

BAADA ya makala iliyopita kwenye safu hii iliyokuwa na kichwa cha habari 'Zama za mwiko mtoto mdogo kula firigisi, mjamzito mayai' ambayo ilikuwa ikielekezea jinsi wazee wa zamani walivyokuwa na sheria, taratibu na kanuni ambazo ziliwakataza watoto kufanya vitu fulani, au kula baadhi ya vyakula, huku kukiwa na mikwara ya vitisho kama vile ukifanya kitu fulani kitatokea kitu fulani, baadhi ya wasomaji wameonekana kuvutiwa na kueleza hisia zao kuhusu hilo.

Hata hivyo kumbe wengi wao ambao kwa sasa ni watu wazima wameonekana kuwa hawakuwa wanapendezewa kabisa, baba kula nyama kubwa, firigisi, kuanza kula yeye kabla ya wengine na hata kumsubiri yeye ndiye ashibe aanze kunawa ndiyo na watoto wakale na waondoke.

Wengi waliopiga simu na kutuma meseji walisema ni kwa sababu ni baba tu na hawakuwa na namna ya kufanya chochote, lakini walikuwa wanatamani mno nao kula firigisi, paja, kiasi kwamba walianza kuuchukia utoto na kutaka kuwa wakubwa ili nao waanze kufaidi ule upendeleo wote wa baba.

Kwenye safu hii leo nitaweka baadhi ya meseji ambazo nimetumiwa na wasomaji wa safu hii ambao wengi wamechangia kwa hisia kali kuhusu utaratibu wa zamani, wakitaja kanuni mbalimbali zisizo rasmi ambazo ziliwekwa na wazee kwa ajili tu ya kutaka mambo yaende sawa.

Pamoja na yote, wote walikubaliana kwamba kilichokuwa kikifanyika na kuwalea kwenye mazingira mazuri, adabu na heshima, lakini hilo walilitambua walipokuwa watu wazima, lakini wakati ule bado wadogo walichokuwa wanaona ni kama wanaonewa hivi na walikuwa 'wanamaindi' baba kuwa kama nahodha wa safari nzima ya msosi, akiwa kama staa wa filamu za kihindi kila kitu anajua yeye.

Kama kawaida, meseji za wasomaji wa safu hii huwa majina yake hayachapishiwi kwa sababu wengi wao hawahitaji kwa sababu sasa ni watu wazima, wenye familia zao, na wengine hadhi kubwa na viongozi kwenye nyanja mbalimbali.

"Kakumbusha sheria ya baba ndio anagawa nyama, utakayopata ndiyo hiyo hiyo, paja lazima ale yeye na kipapatio ndio tunakula watoto." Aliandika msomaji mmoja kutoka Kibaha, mwingine akaandika.

"Kiboko ni ile sheria ya nyama kubwa na zenye mfupa ni za baba, yaani kama nyumbani kwetu ilikuwa hivyo," aliandika mwingine.

"Nakumbuka wakati wa kula kama wali na nyama, baba ndiyo anaanza kunawa, anachukua bakuli la mboga, anamimina mchuzi, akimaliza kumwaga wote mnatakiwa muangalie pembeni akiwa anachagua nyama ya kuanza nayo." Jamaa huyu yuko sahihi kabisa, ila meseji yake inafurahisha sana. Mwingine akaandika.

"Paja kidari cha wakubwa kichwa miguu ndiyo yako mtoto, wa mwisho kula ndiye atakayefagia na kuukunja mkeka."

Meseji nyingine iliandikwa hivi. "Kichwa anakula baba kama ni Samaki, mfupa anakula baba kama ni nyama na Paja au kidari anakula baba, sasa wewe jitie mjanja..." Bado meseji ziliendelea kumiminika kuonyesha watoto wakati huo walivyokua 'wakimaindi' baba kula mapaja ya kuku.

"Paja na firigisi la baba, hakuna kugusa nyama mpaka aanze na hata ukishiba huinuki mpaka baba ashibe nilikuwa nachukia sana."

Meseji moja iliunga mkono tabia za kinababa wa zamani.

"Huo haukuwa ukatili bali tulifunzwa kuwa na nidhamu hata sasa hivi kwenye kizazi cha sasa itokee wageni wale chakula na mwanao halafu aanze kumega tonge na kuwahi paja la kuku kabla ya wakubwa lazma ujisikie vibaya, halafu mbona siyo kinababa tu hata kijana tu akibaki nyumbani na wadogo zake kwenye msosi lazima uwapunje."

Hizi ni baadhi tu ya meseji zilizoonyesha watoto walivyokuwa 'waliwamaindi' baba zao wakati huo, sasa kuna hizi zingine kwenye sheria ya kula hapo zamani.

"Siku ya ubwabwa mchele unachaguliwa saa tisa, chakula kinapikwa saa 11:00, mnaoga mapema hamtoki nyumbani, na ole wako uwaite rafiki zako muda wa kula na hakuna kutangaza mnapika wali, pia kikibaki kidogo anabakishiwa mtoto."

Lakini pia hata staili ya kuitwa kula inabadilika siku ya ubwabwa utasikia "weee Happy shauri yako" bila kumalizia njoo ule.

Meseji moja iliunga mkono tabia za kinababa wa zamani.

Mwingine akatoa mpya kwenye meseji yake.

"Ukikosa nyama unaenda kulia kwa mama uani huku unalia, unapewa nyama na chakula pia."

Mama mmoja akaandika kuwa wakati huo yeye ndiye alikuwa mdogo kwao.

"Mimi ndiyo nilikuwa mtoto, basi nawekewa mpaka kwenye sahani ndugu zangu wasiuvuke ili nishibe kwa sababu wenzangu walikuwa wanakula matonge makubwa, leo nimekuwa mkubwa."

Yupo aliyeandika meseji staili ya kula wakati taa yenyewe ni kibatari.

"Hakikisha taa haizimi na ipo karibu muda wote tukio la likiendelea, na ikizimika tu, mkono unakwenda kuziba nyama isichukuliwe." Meseji ya mwisho imeandiwa hivi.

"Kwetu mtoto ukichukua nyama kubwa utakatwa jicho na mama mpaka utajuta kuzaliwa."

**Tuma meseji 0716 350534**

## Russia yaendelea kuitesa Ukraine

**KYIV,** UKRAINE

VIKOSI vya Russia vimefanya mashambulizi makali katika maeneo tofauti ya Ukraine usiku wa kuamkia jana.

Katika hatua za mapema takribani makombora 17 yamevurumishiwa katika mji wa kusini-mashariki wa taifa hilo wa Zaporizhzhia.

Gavana wa eneo la kusini mwa Ukraine la Udesa, Maksym Marchenko, alisema kumekuwa na mashambulizi ya anga na meli za kivita zilizobeba makombora katika eneo la bahari.

Mashambulizi yamesababisha kelele za ving'ora vya tahadhari hadi asubuhi ya jana hatua ambayo imesababisha maofisa kuwataka raia kujihifadhi kwa hofu ya kutokea mashambulizi mengine zaidi.

Miundombinu muhimu pia imeshambuliwa katika mji wa Khmelnitskyi magharibi Ukraine, Kharkiv kaskazini mashariki na mkoa wa Dnipropetrovsk katikati mwa Ukraine.

Aidha, Waziri wa Mambo ya Kigeni wa Russia, Sergei Lavrov amekutana na watawala wa kijeshi wa Sudan katika kituo cha mwisho cha ziara yake barani Afrika. Lavrov alifanya mazungumzo na Jenerali Abdel Fattah Burhan, mkuu wa Baraza Tawala la Sudan, pamoja na naibu wake Jenerali Mohammed Hamdan Dagalo, anayeongoza kikosi chenye nguvu kinachofahamika kama RSF.

Shirika la habari la Sudan (SUNA) limesema bila kutoa maelezo zaidi kuwa mikutano hiyo ililenga katika kuimarisha ushirikiano kati ya nchi hizo mbili.

Ziara ya Lavrov barani Afrika, ililenga katika kuimarisha mahusiano na kutanua ushawishi katika wakati ambao mataifa ya Magharibi yanataka kuitenga Russia kwa kuiwekea vikwazo kuhusiana na vita nchini Ukraine.

**DW**

# Vita vya maneno yazidisha joto la vita DRC

**KINSHASA,** DRC

VITA vya maneno vinazidi kushika kasi kati ya viongozi wa mataifa ya Rwanda na Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) na kusababisha hali kuzidi kuwa tete.

Juzi Rais wa Rwanda, Paul Kagame, alimtuhumu kiongozi mwenzake wa DRC, Felix Tshisekedi, kwa kuwa kigeugeu kuhusu utekelezaji wa makubaliano kwa lengo la kumaliza mgogoro ulioko mashariki mwa nchi hiyo.

Hata hivyo, Waziri wa Mawasiliano wa DRC, Muyaya Katembwe, hakufurahishwa na kauli hiyo na kueleza Kagame anataka kuhalalisha vitendo viovu vinavyofanywa na wanajeshi wake.

Akizungumza na vyombo vya habari juzi, Muyaya alisema kwamba matamshi ya kiongozi huyo wa Rwanda hayana ukweli wowote na kwamba anataka kuonesha kwamba kile kinachofanywa na wanajeshi wake ni haki.

"Tamko la Luanda lilitumiwa na jumuiya ya kimataifa kama sauti ambayo itaturuhusu kutatua tatizo hilo kwa muda mrefu. Hakuna mahali popote katika hati ya Bujumbura, ambapo taarifa ya Luanda ilitajwa," alisema

Alisema ni juu yake kuendelea na ramani ya barabara ya kutatua tatizo la usalama Mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

"Maneno ya Kagame ni ya kawaida,anayanatoa ili kujaribu kuhalalisha ajenda yake iliyofichwa ambayo inalenga kuweka mashariki mwa DRC katika hali ya kutokuwa na utulivu". aliongeza

Kulingana na Muyaya, Kagame lazima aelewe kwamba mpango wa vurugu umekwisha, lazima sasa kuimarishwa amani.

"Haya ni matamshi yanayomruhusu kuendelea kusababisha madhara. Haki itapatikana hivi karibuni", alisisitiza Waziri huyo.

Wakati huo huo, viongozi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) wamehimizwa kuharakisha uwekaji wa wanajeshi wa ziada katika kikosi cha kikanda kinachotumwa mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo.

Rais wa zamani wa Kenya Uhuru Kenyatta, mpatanishi wa Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) alisema wanajeshi zaidi wanatakiwa kuchukua nafasi katika maeneo ambayo makundi yenye silaha yamejiondoa, kwa mujibu wa makubaliano ya kusitisha mapigano ya Luanda.

Kenyatta alionyesha wasiwasi wake kutokana na kuzorota kwa hali ya usalama katika jimbo la Kivu Kaskazini ambako waasi wa M23 wamepambana na vikosi vya usalama katika wiki za hivi karibuni.

Uganda na Sudan Kusini zinapanga kutuma wanajeshi baada ya wanajeshi kutoka Burundi na Kenya kuwasili mashariki mwa Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo mwaka jana kusaidia kumaliza miongo kadhaa ya ukosefu wa utulivu.

Rais huyo mstaafu wa Kenya alikaribisha wito wa hivi majuzi wa kusitishwa kwa uhasama na pande zote katika mzozo huo na viongozi wa Afrika Mashariki.

Katika taarifa yake, mratibu huyo wa mazungumzo ya amani alisema ataimarisha mipango ya duru ya nne ya mazungumzo jijini Nairobi kwa kuhamasisha uungwaji mkono wa kikanda na kimataifa kwa mkutano huo.

Alizitaka pande zote zinazohusika kuharakisha utekelezaji wa maazimio ya mazungumzo ya tatu ya mashauriano jijini Nairobi.

Pia ameomba msaada wa haraka wa kibinadamu kwa zaidi ya watu nusu milioni waliokimbia makazi yao kutokana na mzozo katika jimbo la Kivu Kaskazini.

Mzozo huo umezorotesha uhusiano na DR Congo, ambayo inaituhumu nchi jirani ya Rwanda kuwaunga mkono waasi wa M23.

**BBC**



Waokoaji wanaondelea kuwasaka watu walionaswa kwenye kifusi, wakifurahi baada ya kumnasua msichana nchini Syria jana: **PICHA: DW**

# Matumaini ya kuwapata watu hai yafifia

**ANKARA-Uturuki**

Zaidi ya watu 20,000 mpaka jana imethibitika wamepoteza maisha katika tetemeko la ardhi lilotokea Jumatatu nchini Uturuki na Syria.

Hata hivyo, Umoja wa Mataifa unaonya kwamba kiwango kamili cha maafa hayo bado hakijafahamika kutokana na majengo mengi yaliyoporomoka bado hajafikiwa.

Waokoaji bado wanatafuta manusura kwenye vifusi, lakini matumaini yanafifia ikiwa ni karibu saa 100 tangu kutokea kwa tetemeko hilo. Hali ya baridi kali inatishia maisha ya maelfu ya walionusurika ambao hawana makazi, maji na chakula. Rais wa Uturuki aliita tetemeko hilo kuwa ni janga la karne.

Juhudi kubwa za kimataifa za kutoa misaada zinaongezeka kwa kasi. Alhamisi Benki ya Dunia iliahidi msaada wa dola bilioni 1.78 kwa Uturuki ikiwa ni pamoja na fedha za haraka kwa ajili ya kujenga upya miundombinu na kusaidia wale walioathiriwa na tetemeko la ardhi.

Mpaka jana maofisa walisema kuwa watu 17,600 wamekufa nchini Uturuki na idadi ya vifo ilikuwa 3,377 nchini Syria.

Idadi hiyo inazidi ile ya zaidi ya 17,000 waliokufa wakati tetemeko kama hilo lilipotokea kaskazini-magharibi mwa Uturuki mwaka 1999.

Makumi ya maelfu ya watu kote Uturuki na Syria wanalala nje kwa usiku wa nne wakijikinga na baridi kali katika makazi ya muda baada ya kukosa makazi kutokana na tetemeko hilo.

**BBC**

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

FORM 58

**THE DISTRIC COURT OF KIGOMA**
**AT KIGOMA**
**PRPBATE AND ADMISTRATION COUSE NO 5 OF 2022**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE**
**NAVINCHAND M. TALATI**
**AND**
**IN THE MATTER OF AN APPLICATION FOR LETTERS OF ADMISTRATION**
**BY**
**FEISAL ISSA KASSAMALI.............APPLICANT**

## GENERAL CITATION
**(Rule 75)**

All persons claiming to have any interest in the estate of the above named deceased a hereby cited to come and see the proceeding if they think fit before the grant probate (or letters of administration) is made to the above named petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 15th day of December, 2022
The will of the said deceased is deposited and open for inspection at the Court
Dated at KIGOMA this 24th day of November, 2022.

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**PROSPER PROSPER PONGO,** Anatangaza kupotea kwa kadi ya Gari aina ya Toyota Land Cruiser, Model No **JTERB71J** Yenye NO za Usajili **T810DZB, CHASSIS NO JTERB71J100016057, ENGINE NO 1HZ0401587. Y**eyote atakaeiona atoe taarifa Kituo chochote cha Polisi. Taarifa ya Polisi **RB NO: DOD/DOD/RB/56751/2023**

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**KWAME DAIMON MWAGA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya gari yenye namba za usajili **T 820 CVV - TOYOTA HARRIER**. Chassis namba **MCU10-0032483.** Engine namba **INZFE5123652.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Control No.: **9910836188411.**

## KUPOTEA KWA KADI YA PIKIPIKI

**HIDAYA BAKARI MSENGA**

anatangaza kupotea kwa kadi ya Pikipiki yenye namba za usajili **MC 942 ARW - SANLG.** Chassis namba **LBRSPJB5XF9011204.** Engine namba **15914029.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi. Taarifa ya Polisi: **DSM/PHQ/RB/51851/2023.**

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**
**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO..... OF 2023**
**IN THE MATTER OF THE ESTATE OF THE LATE GILDA GERALD KATABALWA**
**AND**
**IN THE MATTER OF APPLICATION FOR LETTERS OF ADMINISTRATION**
**BY FRANK GILDA KATABALWA**
**GENERAL CITATION**
**(Rule 75 of Probate Rules)**

**All PERSONS** claiming to have any interest in the estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 15 Day of 02, 2023
Dated at Dodoma this 11 day of January, 2023

MAGISTRATE — RESIDENT MAGISTRATE DODOMA DISTRICT

## TANGAZO LA KUFUNGA KAMPUNI

'WAMILIKI WA KAMPUNI YA JAMES VENTURE GROUP LIMITED (NAMBA YA USAJILI 136135821 YA 19.03.2018) WANAPENDA KUUTANGAZIA UMMA KUWA KAMPUNI YAO IMEFILISIKA NA HIVYO KUAMUA KUIFUNGA KWA MUJIBU WA SHERIA YA MAKAMPUNI BRELA'

## KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BEATUS ELIY KINYONGA**

**ANATANGAZA** kupotelewa na kadi ya GARI yenye namba za usajili **T 458 CQQ.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **RB namba MKB/TR/RB/3111/2023.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA (W) MTWARA**
**MKOA WA MTWARA**
**MAOMBI MADOGO NA 903/2021**
**NMB BANK PLC ........... MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**JOHN ROGGERS RITTE........MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**
**JOHN ROGGERS RITTE, POPOTE ULIPO**,

**UFAHAMU** kwamba shauri hili limepangwa kusikilizwa tarehe 28 Februari, 2023 saa 02:30 asubuhi.
**UNAAMRIWA** kuhudhuria mbele ya Baraza lililopo katika jengo la Braza Idara ya Ardhi Manispaa ya Mtwara siku hiyo bila kukosa, wewe au mwakilishi wako kisheria. Hati ya madai pamoja na vielelezo vingine vyote kuhusiana na shauri hili utavipata kwenye masjala ya Baraza.
**UFAHAMAU KWAMBA** kushindwa kuhudhuria Barazani siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja na kuamuriwa dhidi yako.
Amri hii imetolewa kwa Mkono wangu na <uhuri wa Baraza leo tarehe **17,Januari,2023.**

**KATIKA BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA LA (W) MTWARA**
**MKOA WA MTWARA**
**MAOMBI MADOGO NA 902/2021**
**NMB BANK PLC ........... MLETA MAOMBI**
**DHIDI YA**
**HAWTE INVESTMENT LIMITED........MJIBU MAOMBI**

**KUITWA SHAURINI**
**HAWTE INVESTMENT LIMITED, POPOTE ULIPO**,

**UFAHAMU** kwamba shauri hili limepangwa kusikilizwa tarehe 28 Februari, 2023 saa 02:30 asubuhi.
**UNAAMRIWA** kuhudhuria mbele ya Baraza lililopo katika jengo la Braza Idara ya Ardhi Manispaa ya Mtwara siku hiyo bila kukosa, wewe au mwakilishi wako kisheria. Hati ya madai pamoja na vielelezo vingine vyote kuhusiana na shauri hili utavipata kwenye masjala ya Baraza.
**UFAHAMAU KWAMBA** kushindwa kuhudhuria Barazani siku hiyo shauri litasikilizwa upande mmoja na kuamuriwa dhidi yako.
Amri hii imetolewa kwa Mkono wangu na Muhuri wa Baraza leo tarehe **17,Januari,2023.**

***OFISI ZA MATANGAZO***
***Mikocheni Industial Area, Po.Box 31042, Dar es Salaam.***
***Mobile: +255 - 745 700 710.***
***E-mail: advertise@guardian.co.tz,***
***Website: www.ippmedia.com***

**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi Kwa Bei Poa Tupigie 0677020701**

**TAHADHARI:** Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji **THE GUARDIAN LIMITED** hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.


# HADITHI

# MTAKE MSITAKE-18

MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kiburi cha kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja ya wasichana warembo kijiji hapo ni mmoja ya waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.

**Na Adam Fungamwango : (0716 350534)**

**MAWENI ni moja kati ya vijiji nchini ambavyo vipo mbali na makao makuu ya mkoa. Kutokana na kuwa vipo kilometa nyingi, miundombinu yake na mawasiliano yamekuwa hafifu, kitu ambacho kimewapa baadhi ya viongozi wa kijiji kiburi cha kufanya wanavyotaka. Wameingia mkataba wa kitapeli na kinyonyaji na tajiri aliyejifanya mwekezaji, kuwanyang'anya mashamba wanakijiji na kumuuzia. Badala yake wanakijiji wanalima kwenye ardhi aliyouziwa mwekezaji huyo. Mazao yaliyopatikana anayachukua na kuwalipa wanakijiji hao pesa kidogo ambayo haiwatoshi kujikimu kwa msimu mzima. Tajiri, watoto wake na viongozi wa kijiji pia wamekuwa na tabia ya kunyanyasa kijinsia watoto wa kike. Mary, mmoja ya wasichana warembo kijiji hapo ni mmoja ya waliopata shida hiyo. Hawana pa kupeleka malalamiko, wala wa kumlilia, isipokuwa Mungu tu. Fuatana na mtiririko wa kisa hiki.**




**************************************

"Kifupi niwaelezee kuwa Adel ni Ofisa Usalama Makao Makuu, Dar es Salaam aliyetumwa kuja kuifanya kazi hii na ameifanya kwa kiwango cha hali ya juu sana."

Vilisikika vigelegele kutoka kwa akinamama na mayowe wakimshangilia Adel, kijana ambaye wamekaa naye kiasi cha mwaka mmoja kasoro hivi.

"Adel, Adel, Adel.." Zilisikika sauti. Kuna baadhi ya vijana wachache ambao walikuwa wanataka kupanda jukwaani, lakini walizuiwa na walinzi.

Hata hivyo kuna wengine walishangaa kuona ofisa mzima kama huyo aliyefanya kazi kubwa, lakini akajiingiza kwenye mapenzi na msichana Mary kiasi cha kumwagiwa tindikali, akawa kipofu.

'Mwaka mmoja uliopita mama yake mzazi ambaye ni mwenyeji wa huku alifika na kujionea madudu haya ya uwekezaji mbovu, aliporudi Dar alimuelezea kijana wake ambaye naye aliliwasilisha ofisini na sisi tukamtuma kazi huku ili achunguze na kuleta taarifa sahihi ili tujue la kufanya. Na ndicho leo kilichofanyika.

Mimi nimezungumza sana, sasa namuachia kipaza sauti mwenyewe kwa sababu amesimama sana. Adel sasa zungumza na umati huu, unataka kujua nini ulikuwa unafanya tangu ulipofika hapa hadi kufanikisha kukamatwa kwa Usonzo."

Adel alishikishwa kipaza sauti na akaanza kwa kukohoa kidogo. "Maweni Oyeee." "Oyeee" Sauti ziliitikia kwa nguvu.

"Mimi nisijieleze sana kwa sababu wote mnanijua, nimebakisha miezi kidogo tu ifike mwaka mmoja. Wote jina lake mnalijua, Adel Adam. Kazi yangu ni Ofisa Usalama wa Taifa, nilikuja huku kwa kazi maalum. Kama alivyosema ofisa mwenzangu hapa kwamba mama yangu alikuja huku kumtazama mama yake mzazi, akakutana na vitimbi vya uwekezaji wa Usonzo, akiwanyang'anya ardhi wanakijiji. Robo tatu yote ilichukuliwa naye. Akawa anawalimisha na kuwapa ujira mdogo. Mama aliporudi aliniambia hilo. Nikaliwasilisha ofisini. Wakanipa kazi hii. Nitakujaje? Nikaja kama nimekuja kumchukua bibi yangu mgonjwa, lakini nilitengeneza mazingira ya kwamba hachukuliki ili niendelee kuishi hapa kwa makusudi.

**Wakati akiongea maneno hayo watu walikuwa kimya, wengine wakionyesha mshangao kwa kile walichokuwa wakikisikia.**

Kazi yangu kubwa ilikuwa ni kukusanya taarifa zote na kuzipeleka Makao Makuu. Nikuambieni ukweli tu hata nyaraka zote ninazo. Zote ambazo viongozi wa kijiji walisainiana na mwekezaji zipo mikononi mwetu..." Kabla hajaendelea vigelegele vilisikika.

"Kwa hiyo upo ushahidi wa kutosha na hili litapelekwa mahakamani, wala msiwe na shaka haki itatendeka." Wanakijiji wakashangilia tena.

"Vingi tayari wameshasema wenzangu, hapa watu sasa labda wangetaka kujua kuwa nyaraka hizi nimezipata vipi wakati zilikuwa zinatunzwa kwenye ulinzi wa hali ya juu kwenye ofisi za Usonzo. Pia undani wa mimi kuwa kipofu.

Nilipokuja hapa pamoja na mambo mengine nilibahatika kuzoeana na msichana Mary, yule pale. Kuzoeana naye kulisababisha wengi wakasema kuwa ni mpenzi wake. Lakini wakati huo huo mwekezaji naye alikuwa anamtaka msichana huyo, ila mwenyewe alikuwa anakataa.

Urafiki wangu na Mary ulimkera sana Usonzo na akatengeneza mpango wa kutaka kuniua. Alishangaa kuona Mary alikuwa anamkataa yeye mwenye pesa, lakini amemkubali kijana wa kawaida aliyetoka mjini. Nilitaka kuuawa siyo kwa sababu ya kugundua kuwa mimi ni hatari kwao kama mwanausalama, bali ni mapenzi.

Kikao kilifanyika nikamatwe, nilazishwe kuondoka, au niuawe. Niliwasiliana na Makao Makuu na wakaniambia nifanye chochote kile lakini nisiondoke hadi nikamilishe misheni, lakini nizuie nisitekwe, kufukuzwa wala kuuawa. Pamoja na hayo walinionya nisizuie vitu hivyo kwa kutumia nguvu, labda kupambana nao, bali akili na hila zaidi kwa sababu hawakutaka yoyote yule ahisi labda mimi si mtu wa kawaida."

Wakati akiongea maneno hayo watu walikuwa kimya, wengine wakionyesha mshangao kwa kile walichokuwa wakikisikia.

"Mpango namba moja nilioona unafaa ni kujifanya kipofu. Siku zote ambazo mlidhani kwamba mimi ni kipofu si kweli. Ulikuwa ni mpango mkakati ili Usonzo asiniteke wala kufanya chochote kwangu ili niendelee kuifanya kazi ya upelelezi kwa amani na uhuru zaidi. Ukweli uliokuwepo hapa mimi si kipofu."

Alisema na kuvua mawani yake. Aliweka fimbo yake pembeni na kushuka chini kwa kasi akipiga hatua moja moja kwenye ngazi na kupandisha tena.

Hili lilisabisha umati wote ulipuke kwa nderemo na vifijo, huku baadhi walionekana kama wanaangalia filamu, wasiamini kile kilichotokea.

Aliporudi kila kitu alikiweka pembeni. Sasa aliongea kama mtu mzima na si mlemavu wa macho tena. Miwani aliweka pembeni.

"Jamani mpango huu niliufanya kwa kushirikiana na Mary kwa ajili ya kumzuga Usonzo na kweli alizugika na ilisaidia kwa pande zote mbili. Nilimwambia Mary najifanya kipofu na yeye ndiye ionekane amenimwagia tindikali ili wote wawili, mimi na yeye tuishi kwa amani kwenye kijiji kwa sababu alituchukia na alikuwa kama anataka kufanya kisasi, hivyo habari hii angeonekana kufurahishwa na tukio hili. Na kweli ndivyo ilivyokuwa."

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# SIMBA QUEENS YAONGOZA LIGI, YATAMBA HAWASHIKIKI

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kukaa kileleni kwa mara ya kwanza msimu huu kutokana na ushindi wa mabao 4-1 walioupata dhidi ya Baobab Queens kutoka Dodoma katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa juzi, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, amesema bado safu yake ya ushambuliaji inatakiwa kuongeza umakini.

Ushindi huo umewafanya mabingwa watetezi wa ligi hiyo, Simba Queens kufikisha pointi 19 na nafasi ya pili sasa inashikiliwa na JKT Queens yenye pointi 18 na Yanga Princess yenye alama 17 ikifuatia.

Akizungumza na gazeti hili jana, Lukula, alisema anaamshukuru Mungu kupata ushindi katika mechi hiyo na kuongeza sasa kila mchezo kwao ni sawa na fainali.

Lukula alisema pia anafurahi kuona timu yake inapata ushindi mnono licha ya ligi hiyo kutokuwa nyepesi.

Kocha huyo aliongeza kuwa kikosi chake kitaendelea kujituma katika kila mechi kwa sababu wanahitaji kufikia malengo yao.

"Ligi ya msimu huu ni ngumu na ukiangalia msimamo wake utaona hata aliyekuwepo katika nafasi ya sita anaweza kufanya vizuri, tuna kazi kubwa ya kupambana katika kila mechi ili kutafuta ushindi na kutetea ubingwa wetu.

Hii mechi tulicheza kama fainali kwa sababu tusipokuwa makini hatutafikia malengo yetu, mabadiliko ya kikosi yanatokana na baadhi ya wachezaji wametumika sana kwa kucheza michezo mingi bila ya kupumzika," alisema kocha huyo.

Alimtaja Asha Djafar ambaye alicheza muda mrefu mechi za ligi, michuano ya CECAFA na Ligi ya Mabingwa Afrika na alicheza mechi za kwanza msimu huu na sasa ameamua kumpumzisha na kuwapa nyota wengine nafasi ya kucheza.

Mshambuliaji wa timu hiyo, Mwanahamisi Omary 'Gaucho', alisema kitendo cha wao kukaa kileleni wapinzani wasahau suala la kushuka katika nafasi hiyo.

Gaucho alisema kitendo cha kukaa kileleni kimewaongezea nguvu ya kupambana ili kufikia malengo yao makubwa ya kutetea ubingwa wanaoushikilia.

"Ligi ni ngumu , lakini kwa kuwa tuko kileleni basi wajue kazi wanayo kutushusha, kwa sasa tumefika katika nafasi yetu na kazi iliyopo ni kupambana kila mechi kutafuta matokeo chanya ili kufikia malengo yetu," alisema Gaucho.

Mabao ya ushindi katika mechi ya juzi yalifungwa na Vivian Corazone aliyetikisa nyavu mara mbili, Jentrix Shikangwa na Oppa Clement.

Simba Queens itashuka tena dimbani Februari 14, mwaka huu kuwakaribisha Ceassia Queens kutoka Iringa.




Mshambuliaji wa Simba Queens, Jentrix Shikangwa (kushoto), akipambana kuwania mpira dhidi ya mchezaji wa Baobab Queens katika mechi ya Ligi Kuu ya Wanawake Tanzania iliyochezwa kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam juzi. Simba Queens ilishinda mabao 4-1. **PICHA: SIMBA SC**

## Wanawake waitwa kupima afya Machi 8

**Na Saada Akida**

WANAMICHEZO wanawake kutoka sehemu mbalimbali nchini wametakiwa kujitokeza kupima afya zao Machi 8, mwaka huu kwenye Ukumbi wa Diamond Jubilee jijini, Dar es Salaam.

Akizungumza na gazeti hili jana, Mratibu wa pambano la ngumi lijulikanalo kwa jina la Malkia wa Ulingo, Khadija Hamisi, alisema lengo la kuandaa zoezi hilo ni kuhakikisha afya za wanamichezo wanawake zinakuwa imara.

Khadija alisema wanamichezo wanawake wanatakiwa kutambua thamani yao, hivyo kujitokeza kufanya vipimo hivyo kutawaweka kwenye nafasi nzuri ya kuendeleza vipaji vyao.

Alisema zoezi hilo la upimaji afya lifanyika kwa muda wa siku tatu kabla ya pambano la Malkia wa Ulingo ambalo mabondia wanaoshiriki watachuana ifikapo Machi 11, mwaka huu hapa jijini.

"Zoezi hilo la upimaji afya linahusisha wanawake wote wanaoshiriki michezo mbalimbali hapa nchini ikiwamo mpira wa kikapu, mpira wa wavu, mpira wa miguu na mabondia wa kike," alisema Khadija.

Aliongeza uamuzi huo wa kuwapima afya wanamichezo wanawake unalenga kutoa nafasi kwa wanamichezo hao kujua hali zao za kiafya, lakini pia watapata mafunzo yatakayowajenga kisaikolojia.

"Hili zoezi litaanza kufanyika katika siku ya wanawake duniani kwa sababu kuna wanawake wengi ambao wako katika michezo mbalimbali ikiwemo ngumi na soka kujiweka tofauti, elimu itakayotolewa itawasaidia kuwabadilisha hasa kwa watoto wetu wakike kujiweka vizuri," alisema Khadija.

Aliwataka wanamichezo wenye ulemavu pia kujitokeza katika zoezi hilo ambalo litawasaidia kufahamu na kutatua changamoto zilizojificha.

Katika usiku wa Malkia wa Ulingo, pambano kuu litamkutanisha Mtanzania, Stumai Muki dhidi ya Chimwemwe Banda kutoka Malawi ambao watawania mkanda wa ubingwa unaotambuliwa na Shirikisho la Ngumi la Kimataifa la UBO wakati Najma Isike atapigana na Happy Daudi.

# Kabbadi Taifa kuingia kambini Dar

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya Taifa ya Kabbadi inatarajiwa kuingia kambini hivi karibuni kwa ajili ya kujiandaa na mashindano ya Kombe la Dunia yatakayofanyika baadaye mwaka huu huko India, imeelezwa.

Kikosi cha timu hiyo kitajulikana baada ya kumalizika kwa Ligi ya Taifa ya mchezo huo itakayofanyika kuanzia Februari 22, mwaka huu jijini, Dar es Salaam.

Mwenyekiti wa Chama cha Kabbadi Tanzania, Abdallah Nyoni, aliliambia gazeti hili maandalizi ya ligi hiyo yako katika hatua za mwisho na wanaamini watapata vikosi imara vitakavyokwenda kuiwakilisha vyema nchi.

Aliongeza wanashukuru kuingia mkataba na Chuo Kikuu cha Mtakatifu Joseph wenye lengo la kusaidia kambi ya timu hiyo.

"Tunakishukuru Chuo cha Mtakatifu Joseph kwa kuamua kushirikiana na sisi kuiwezesha timu yetu ya taifa kujiandaa na mashindano ya dunia. Mkataba tulioingia utasaidia gharama za kambi, chakula, malazi, usafiri wa ndani pamoja na kutoa mafunzo mbalimbali kwa walimu, waamuzi, wachezaji na waandishi wa habari," Nyoni alisema. Makamu Mwenyekiti wa Chuo cha Mtakatifu Joseph, Prof. Elius Zephania, alisema kwa sasa wameamua kuwekeza kwenye taaluma pamoja na shughuli mbalimbali za kijamii ikiwamo kuendeleza mchezo huo.

"Tunakishukuru Chama cha Kabbadi kukubali kufanya kazi pamoja na sisi tutawasaidia gharama kama chakula malazi vile vile tutawapatia ofisi nzuri ambayo itakuwa jijini Dar es Salaam,alisema Zephania.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

### CHIWELL ATAKIWA CITY

KLABU ya Manchester City inataka ya kumsajili beki wa kushoto wa Chelsea na Timu ya Taifa ya England, Ben Chilwell mwenye umri wa miaka 26 katika dirisha la usajili la msimu wa joto. (***CaughtOffside***)

### OSIMHEN ANUKIA CHELSEA

CHELSEA imemweka mshambuliaji wa Napoli na Timu ya Taifa ya Nigeria, Victor Osimhen, mwenye umri wa miaka 24, kama kipaumbele chao kikuu katika dirisha la usajili la majira ya kiangazi. (***90MIN***)

### SPURS YAMTAKA GUEHI

KLABU ya Tottenham Hotspur inavutiwa na beki wa Crystal Palace, Marc Guehi, mwenye umri wa miaka 22, wakati huu wakitaka kusajili mabeki wawili wapya wa kati kwa ajili ya msimu ujao. (***Mail***)

### LEIPZIG MACHO KWA KEITA

RB Leipzig huenda ikatafuta kumsajili tena kiungo wa kati, Naby Keita mwenye umri wa miaka 27 katika msimu wa joto baada ya siku ya mwisho ya usajili wa Januari kukataliwa na Liverpool kumwachia mchezaji huyo wa kimataifa wa Guinea. (***Bild***)

### KESSIE ALIIKATAA SPURS

KIUNGO wa kati wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Ivory Coast, Franck Kessie, mwenye umri wa miaka 26 alikataa kuhamia Tottenham Hotspur katika dirisha la uhamisho la Januari. (***Sport***)

### LUKAKU KUBAKIA INTER

INTER Milan ipo tayari kufanya mazungumzo zaidi na Chelsea kuhusu mkataba wa kudumu wa kumnunua mshambuliaji wa Ubelgiji, Romelu Lukaku. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 29 kwa sasa yuko kwa mkopo katika klabu hiyo ya Serie A. (***Gazzetta dello Sport)***

### WARD KUTUA AJAX

AJAX inazidisha juhudi zao za kumpata Mkurugenzi wa Michezo wa Liverpool, Julian Ward, ambaye anatajwa anafikiria kuachana na majukumu yake ndani ya Anfield mwishoni mwa msimu huu. (***Telegraph***)

### SLOT AKARIBIA LEEDS

LEEDS United inafikiria kumchukua Kocha wa Feyenoord, Arne Slot ili kuiongoza timu hiyo. (***Times***)

### BUSQUETS, BARCA SAFI

BARCELONA inataka kuongeza mkataba wa nahodha na kiungo wa zamani wa Timu ya Taifa ya Hispania, Sergio Busquets mwenye umri wa miaka 34. (***Mundo Deportivo)***

### HALL ANUKIA LIVERPOOL

LIVERPOOL inamfuatilia kwa karibu nyota wa Birmingham City na Timu ya Taifa ya England ya vijana, George Hall. Everton na Leeds pia zinavutiwa na kiungo huyo mwenye umri wa miaka 18. (***Football Insider***)


### PAVARD KUTUA BARCA

BARCELONA itafuatilia mpango wa kumnunua beki wa kulia wa Bayern Munich na Timu ya taifa ya Ufaransa, Benjamin Pavard, mwenye umri wa miaka 26 katika majira ya msimu wa joto. (***Mundo Deportivo***)

### ANCELOTTI ATAJWA BRAZIL

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti huenda akachukua nafasi ya Tite kama Kocha Mkuu wa Brazil. (***GeGlobo,via Defensa Central***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# TEN HAG : RASHFORD AZALIWA UPYA UNITED

**MANCHESTER,** England

**Ni kutokana na kuonyesha kiwango cha juu na pia amekuwa chanzo cha...**

KIWANGO bora cha Marcus Rashford ndio ufunguo wa Manchester United iliyojaa "watu mahiri na wenye furaha", kwa mujibu wa Kocha, Erik ten Hag.

**Mchezaji huyo wa kimataifa wa England alivumilia msimu mgumu wa 2021-22, lakini ni mshambuliaji aliyezaliwa upya chini ya Mholanzi huyo pale Old Trafford msimu huu.**

Rashford aliiokoa United na kuiwezesha kupata pointi moja kwenye sare ya 2-2 dhidi ya Leeds United hapo juzi, akifunga bao lake la 11 la Ligi Kuu England msimu huu.

Ten Hag anashukuru mabadiliko yake kwa kuongeza umakini ndani na nje ya uwanja, na ameongeza kuwa amekuwa na mchango mkubwa kwa wachezaji wenzake.

"Ana umakini mkubwa kwa wakati huu," alisema Ten Hag akiiambia Sky Sports kuhusu Rashford.

"Anafahamu hilo, akifanya harakati sahihi yeye au timu yake itamfikisha katika nafasi nzuri ya kufunga mabao.

"Kwa wakati huu, anaweka mtiririko, analeta kila mchezo uwanjani, ikiwa ana nguvu na viwango hivyo, atafunga mabao.

"Kitu pekee ambacho timu inapaswa kufanya ni kumweka katika nafasi hiyo."

Ten Hag aliongeza: "Tunaona watu waangalifu na wenye furaha, nadhani lazima tuendelee kuwa chanya. Unapaswa kukabiliana na mchezo kwa mtazamo chanya."

Rashford ndiye mfungaji bora wa United msimu huu, akisaidia kuziba pengo la Cristiano Ronaldo aliyejiondoa katika klabu hiyo katikati ya msimu.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SUPA JACKPOT KWA 1000/- 1,074,7

MECHI KALI
ARSENAL
VERSUS
BRENTFORD
1 | 1.44
X | 4.28
2 | 6.52

KUWEKA PESA:
- PIGA *150*87#, CHAGUA 4
- WEKA PESA.
tigo pesa
vodacom m-pesa
halopesa
airtel money
SEND

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
PIGA *150*87#
GBT:0249 HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, PIGA:
0764115588, 0677115588
0685115588
18+
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa



# RONALDO AFIKISHA MABAO 500

**RIYADH,** Saudi Arabia

CRISTIANO Ronaldo alifunga bao la 500 la ligi katika maisha yake kwenye ushindi wa mabao 4-0 wa Al Nassr dhidi ya Al Wehda.

Nahodha huyo wa Ureno alifunga mabao yote manne huku klabu yake mpya ikipanda kileleni katika Ligi ya Saudia kwa tofauti ya mabao.

Akiwa amefungua akaunti yake ya mabao kwa Al Nassr katika sare ya 2-2 dhidi ya Al Fateh mara ya mwisho, bao muhimu la Ronaldo lilipatikana dakika ya 21 baada ya kuachia shuti hafifu lililompita Abdulquddus Atiah.

Aliongeza bao la pili na alikamilisha hat-trick yake kwa mkwaju wa penalti dakika ya 53, kabla ya kupata bao lake la nne na kumalizia ushindi mnono baada ya dakika ya 30.

Ronaldo na Al Nassr watarejea uwanjani Ijumaa ijayo, watakapowakaribisha Al Taawoun kwenye Uwanja wa Chuo Kikuu cha King Saud.

# Guardiola, Ancelotti, Scaloni wawania tuzo

**PARIS,** Ufaransa

KOCHA wa Argentina aliyeshinda Kombe la Dunia, Lionel Scaloni na Carlo Ancelotti wa Real Madrid ni miongoni mwa walioingia fainali ya kuwania tuzo ya Kocha Bora wa FIFA wa Wanaume ya mwaka 2022.

Wawili hao wameorodheshwa pamoja na Pep Guardiola wa Manchester City katika nafasi tatu za mwisho.


Scaloni, ambaye alimaliza nafasi ya nne mwaka jana, aliiwezesha Argentina, La Albiceleste, kushinda Kombe la Dunia nchini Qatar 2022 na anatambulika kwa juhudi zake za kusaidia kutinga fainali ya Kombe la Dunia kwa mara ya kwanza tangu mwaka 1986.

Ancelotti alifanya kazi nzuri akiwa na Real Madrid, baada ya kushinda mataji mawili Ligi ya Mabingwa Ulaya na Ligi Kuu Hispania maarufu LaLiga.

Guardiola aliiongoza City kutwaa ubingwa mwingine wa Ligi Kuu England, ingawa alishindwa katika Ligi ya Mabingwa Ulaya kwa mara nyingine tena na kuona mpinzani wake Liverpool akinyakua Kombe la FA na lile la EFL.

Kwa upande wa tuzo ya Kocha Bora wa FIFA wa Wanawake, Kocha wa England, Sarina Wiegman ametajwa kuwania nafasi hiyo akichuana na Kocha wa Brazil, Pia Sundhage.

Washindi wa tuzo Bora za Soka za FIFA watatangazwa Februari 27.



741,067/-

SUPA JACKPOT
MECHI WIKI HII
BASHIRI KWA USAHIHI MECHI ZOTE

| TAREHE | MUDA | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 01. 11/02/23 | 18:00 | Southampton FC vs Wolverhampton Wanderers | 2.75 | 3.10 | 2.60 |
| 02. 11/02/23 | 18:00 | KVC Westerlo vs KAA Gent | 2.80 | 3.30 | 2.42 |
| 03. 11/02/23 | 18:15 | UD Almeria vs Real Betis Seville | 2.80 | 3.30 | 2.44 |
| 04. 11/02/23 | 22:45 | Lazio Rome vs Atalanta BC | 2.27 | 3.35 | 3.00 |
| 05. 11/02/23 | 23:00 | Valencia CF vs Athletic Bilbao | 2.95 | 3.15 | 2.41 |
| 06. 12/02/23 | 09:00 | Macarthur FC vs Wellington Phoenix FC | 2.55 | 3.15 | 2.29 |
| 07. 12/02/23 | 15:00 | Toulouse FC vs Stade Rennes | 3.05 | 3.35 | 2.25 |
| 08. 12/02/23 | 16:00 | Getafe CF vs Rayo Vallecano | 2.75 | 2.85 | 2.80 |
| 09. 12/02/23 | 16:30 | Vitesse Arnhem vs FC Utrecht | 2.39 | 3.45 | 2.75 |
| 10. 12/02/23 | 17:00 | Angers SCO vs AJ Auxerre | 2.25 | 3.30 | 3.10 |
| 11. 12/02/23 | 17:00 | Montpellier HSC vs Stade Brest 29 | 2.35 | 3.25 | 2.95 |
| 12. 12/02/23 | 17:30 | Hertha BSC vs Borussia Monchengladbach | 2.75 | 3.50 | 2.37 |
| 13. 12/02/23 | 18:15 | RC Celta de Vigo vs Atletico Madrid | 3.40 | 3.05 | 2.24 |
| 14. 12/02/23 | 19:30 | 1. FC Cologne vs Eintracht Frankfurt | 2.65 | 3.45 | 2.47 |
| 15. 12/02/23 | 20:30 | Real Valladolid vs CA Osasuna | 2.60 | 3.05 | 2.80 |
| 16. 12/02/23 | 21:00 | Sporting Lisbon vs FC Porto | 2.75 | 3.20 | 2.55 |
| 17. 12/02/23 | 22:45 | Olympique Lyon vs RC Lens | 2.39 | 3.40 | 2.80 |

MECHI ZA USHINDI
"1" NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA "X" NI TIMU KUTOKA SARE "2" NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMAMOSI - 11/02/2023

| MUDA | GAME ID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 15:30 | 2851 | West Ham vs Chelsea | 3.27 | 3.12 | 2.21 |
| 16:00 | 1198 | Forest Rangers vs Chambishi FC | 1.72 | 3.07 | 5.20 |
| 16:00 | 3458 | Mtibwa Sugar vs Dodoma FC | 2.09 | 2.75 | 3.35 |
| 16:00 | 4008 | EN Paralimni vs Apoel Nicosia | 6.82 | 3.89 | 1.50 |
| 16:00 | 4404 | Beitar Jerusalem vs FC Ashdod | 2.34 | 3.26 | 2.74 |
| 16:00 | 4626 | FC Muza vs Napsa Stars | 2.61 | 2.66 | 2.93 |
| 16:20 | 1308 | Dubba Al-Husun vs City Football Club | 1.14 | 5.80 | 11.00 |
| 16:20 | 1580 | Masafi vs Masfoot Sports Club | 2.40 | 3.05 | 2.55 |
| 16:20 | 3809 | AL Jazira AL Hamra vs AL-Rams | 1.98 | 3.55 | 2.85 |
| 16:25 | 4463 | Baynounah vs Fursan Hispania FC | 2.02 | 3.42 | 3.21 |
| 17:00 | 2737 | Empoli vs Spezia | 2.00 | 3.36 | 3.56 |
| 17:00 | 5568 | CF Estrela vs Benfica Lisbon B | 1.71 | 3.79 | 4.21 |
| 17:30 | 1040 | Hoffenheim vs Bayer Leverkusen | 2.88 | 3.43 | 2.27 |
| 17:30 | 2000 | Bayern Munchen vs VfL Bochum | 1.10 | 8.68 | 16.77 |
| 17:30 | 3028 | Werder Bremen vs Borussia Dortmund | 3.86 | 3.96 | 1.76 |
| 17:30 | 3253 | SC Freiburg vs Stuttgart | 1.80 | 3.58 | 4.08 |
| 17:30 | 5619 | Mainz vs Augsburg | 1.77 | 3.71 | 4.06 |
| 18:00 | 2142 | Crystal Palace vs Brighton | 3.62 | 3.37 | 1.97 |
| 18:00 | 2446 | Fulham vs Nottingham | 1.88 | 3.42 | 3.91 |
| 18:00 | 2775 | Ayr United vs Elgin City | 1.39 | 4.46 | 6.43 |
| 18:00 | 3563 | Leicester vs Tottenham | 3.16 | 3.46 | 2.11 |
| 18:00 | 4255 | Arsenal vs Brentford | 1.44 | 4.28 | 6.52 |
| 18:00 | 5327 | Southampton vs Wolverhampton | 2.83 | 3.08 | 2.48 |
| 18:15 | 1736 | Zaragoza vs Alaves | 2.68 | 2.83 | 2.83 |
| 18:15 | 4239 | Almeria vs Betis | 2.80 | 3.25 | 2.46 |
| 18:30 | 2428 | Al Ahly Cairo vs Flamengo | 4.66 | 3.99 | 1.58 |
| 18:30 | 2680 | Hapoel Beer Sheva vs Hapoel Katamon | 1.56 | 3.73 | 5.18 |
| 19:00 | 1569 | Monaco vs Paris St Germain | 2.54 | 3.48 | 2.54 |
| 19:00 | 5113 | Wolfsberger AC vs WSG Wattens | 1.94 | 3.53 | 3.32 |
| 19:00 | 5142 | RB Salzburg vs Austria Lustenau | 1.17 | 6.23 | 11.42 |
| 19:30 | 2177 | AS Dakar Sacre Coeur vs Generation Foot | 2.52 | 2.58 | 3.17 |
| 19:30 | 2335 | Sectzya Nes Ziona vs Hapoel Haifa | 3.00 | 3.20 | 2.20 |
| 19:30 | 3222 | Bnei Sakhnin vs Maccabi Bney Reine | 2.17 | 3.16 | 3.11 |
| 19:30 | 3776 | ASC Diambars vs US Goree | 1.93 | 2.90 | 4.24 |
| 19:30 | 4258 | Teungueth vs Stade De Mbour | 2.14 | 2.70 | 3.84 |
| 20:00 | 2328 | Talaea El Gaish vs El Daklyeh | 1.97 | 2.99 | 4.28 |
| 20:00 | 3788 | Lecce vs Roma | 4.15 | 3.21 | 1.90 |
| 20:30 | 1727 | Bournemouth vs Newcastle | 5.77 | 3.93 | 1.53 |
| 20:30 | 2445 | RB Leipzig vs Union Berlin | 1.70 | 3.57 | 4.76 |
| 20:30 | 3468 | Maccabi Haifa vs Ironi Kiryat Shmona | 1.29 | 4.99 | 8.10 |
| 20:30 | 5497 | Sevilla FC vs Mallorca | 1.93 | 3.09 | 4.39 |
| 20:45 | 4367 | NEC Nijmegen vs Cambuur | 1.70 | 3.62 | 4.66 |
| 21:00 | 3012 | FC Arouca vs Santa Clara | 2.11 | 3.23 | 3.43 |
| 21:00 | 4277 | PAS Giannina vs Ionikos Nikea FC | 1.93 | 3.24 | 4.03 |
| 22:00 | 4566 | Real Madrid vs Al Hilal Riyadh | 1.25 | 5.37 | 8.87 |
| 22:00 | 5890 | PSV Eindhoven vs Groningen | 1.14 | 7.34 | 14.88 |
| 22:45 | 3751 | Lazio vs Atalanta | 2.35 | 3.27 | 2.87 |
| 23:00 | 3002 | Clermont Foot vs Marseille | 4.78 | 3.63 | 1.69 |
| 23:00 | 4674 | Valencia vs Athletic Bilbao | 2.95 | 3.15 | 2.41 |
| 23:00 | 5830 | Las Palmas UD vs Lugo | 1.42 | 4.07 | 7.74 |

CHEZA KWA WAJIBU. KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

# WABRAZIL WA SINGIDA BS WALIA NA UMBALI MREFU

**Na Adam Fungamwango**

UONGOZI wa Singida Big Stars umesema moja ya changamoto wanayoipata wachezaji wao wa kigeni kutoka Brazil, Bruno Gomes (pichani), na Rodrigo Fegu, ni kutozoea kusafiri umbali mrefu, imefahamika.

Kocha Msaidizi wa Singida Big Stars, Mathias Lule, aliliambia gazeti hili wachezaji hao wanapata tabu sana wanaposafiri kwa umbali mrefu kutoka sehemu moja hadi nyingine kwa ajili ya kwenda kucheza mechi za Ligi Kuu Tanzania Bara.

Lule alisema nyota hao bado hawajazoea hali hiyo na inawapa ugumu huku ikichangia kuathiri viwango vyao kutokana na uchovu wanaopata.

"Sisi Singida Big Stars hatugombanii nafasi yoyote katika Ligi Kuu Tanzania Bara, malengo tuliyojiwekea ni kucheza vizuri kupata matokeo chanya kwenye kila mchezo tunaocheza, lakini klabu haijaweka malengo wala kutuwekea makocha malengo, ila kwa jinsi tunavyokwenda tutafikia pazuri.

Ila tuna changamoto moja kwenye timu yetu, Wabrazil hawajazoea ligi ya Kitanzania, hapa tunasafiri sana tena umbali mrefu, kilomita nyingi kwao hawajazoea, hiyo imekuwa changamoto kubwa inayosababisha hata viwango vyao kupanda na kushuka," Lule alisema.

Kuhusu mechi hiyo, Lule alisema itakuwa ngumu kwa sababu Ihefu kwa sasa imepata ushindi mfululizo, hali ambayo imewajengea uwezo wa kujiamini wachezaji wake.

Singida Big Stars kwa sasa iko jijini Mbeya ikijiandaa na mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara dhidi ya Ihefu itakayochezwa kesho kwenye Uwanja wa Highland Estates, Mbarali.




## Simba yakamilisha hesabu za ushindi

INATOKA UK 24

"Tunaitakia kila la heri klabu ya Yanga, inayocheza michezo ya shiriko tarehe 12, Februari huko Tunisia, ujumbe wetu kwao, tetemesha Watunisia, tunaitakia heri nyingi sana Simba, Wekundu wa Msimbazi wanaocheza michezo ya Klabu Bingwa Afrika huko Guinea tarehe 11 Februari, 2023.

Ujumbe wetu kwenu nyunyiza hao Waguinea walale mabao mengi kwao. Hakuna mashaka na viwango vyenu, Simba nyie ni miongoni mwa klabu 10 bora Afrika." alisema Waziri Mkuu.

Baada ya mchezo huo, Simba itarejea nyumbani kuwasubiri Raja Casablanca kwa ajili ya mchezo wa pili wa Kundi C utakaochezwa Februari 18, mwaka huu kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam.

## Yanga yafunguka

INATOKA UK 24

wapinzani wetu wanahitaji ushindi kitu ambacho tutakifanya ni kupambana zaidi," alisema Kaze.

Kocha huyo aliongeza wamejipanga kuongeza umakini na wamewataka mashabiki wao kutokuwa na hofu.

Alisema pia kukosekana kwa baadhi ya wachezaji wao isiwaumize kwa sababu kila nafasi ina mchezaji mbadala ambaye ana uwezo wa kufanya vizuri na kuisaidia timu.

Naye mshambuliaji wa timu hiyo, Fiston Mayele, alisema wamefanya mazoezi magumu na wanauhakika wa kufanya vizuri katika mchezo huo wa keshona kuifanya safari yao kuwa nyepesi.

"Malengo yetu ni kufanya vizuri katika mchezo huo kwa sababu ni mechi yetu ya kwanza, huu mchezo ndio unaotupa taswira ya michezo yetu ijayo, kikubwa tuko tayari kwa ajili ya kusaka matokeo mazuri," alisema Mayele.

Wakati huo huo, kipa namba mbili wa Yanga, Abdultwalib Mshery, ambaye yuko katika mji wa Suusse, Tunisia kwa ajili ya matibabu ya jeraha lake la goti tayari amefanyiwa upasuaji na anaendelea vizuri.

"Nashukuru Mungu tayari operesheni yangu imeenda vizuri na naendelea vizuri, ninaimani baada ya muda nitarejea katika hali yangu ya kawaida na ubora wangu katika majukumu ya kuipigania klabu yangu ya Yanga," alisema Mshery.

# Michezo

Nipashe

Jumamosi Februari 11, 2023




Ten Hag : Rashford azaliwa upya United

UKURASA 21



Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliviera maarufu Robertinho (kulia), akiwa na wasaidizi wake baada ya kuwasili katika mji wa Conakry, Guinea kwa ajili ya kuwakabili wenyeji Horoya AC kwenye mchezo wa Kundi C wa mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika utakaochezwa leo. **PICHA: SIMBA SC**

## Yanga yafunguka Monastir watalala

**Na Saada Akida**

USHINDI ndio neno ambalo wachezaji, makocha na viongozi wa Yanga wanahitaji kulisikia baada ya kutua salama katika jiji la Tunis, Tunisia tayari kwa mchezo wa Kombe la Shirikisho Afrika dhidi ya US Monastir.

Yanga inatarajia kuwakabili US Monastir katika mechi ya kwanza ya Kundi D itakayochezwa kwenye Uwanja wa Olympique Hammadi Agrebi.

Kocha Msaidizi wa Yanga, Cedric Kaze, aliliambia gazeti hili kikosi chao kimeendelea kujiimarisha na jana kilifanya mazoezi ambayo yatawaweka tayari kwa mchezo huo ambao wanahitaji kuanza vyema hatua ya makundi.

Kaze alisema Yanga inahitaji pointi zote tatu na wamejipanga kucheza soka la kiwango cha juu kwa sababu wanahitaji kutimiza malengo.

Aliongeza kupata ushindi katika mchezo huo kutawapata mwanga mzuri kuelekea michezo iliyopo mbele yao katika michuano hiyo inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF).

"Wachezaji wanatambua umuhimu wa kushinda mechi ya kwanza, tutahakikisha wanapambana kwa lengo la kutafuta alama muhimu katika mchezo huu ili kufikia malengo yetu ni kukusanya alama nyingi na kufuzu kucheza robo fainali.

Ukweli ushindani ni mkubwa na tunajua

INAENDELEA UK 23

# SIMBA YAKAMILISHA HESABU ZA USHINDI

## ●●● Yashuka ugenini Guinea, serikali yawatakia heri watani wa jadi...

**Na Adam Fungamwango**

KAZINI, Simba inatarajia kuwavaa wenyeji Horoya AC katika mechi ya hatua ya makundi ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Jenerali Lansana Conte ulioko jijini Conakry, Guinea.

Mechi hiyo itachezwa kuanzia saa 1:00 usiku kwa saa za Tanzania.

Hata hivyo itakuwa ni mechi ya pili katika Kundi C baada ya mechi ya kwanza iliyochezwa jana usiku kwenye Uwanja wa Mohamed wa Tano, Morocco kati ya Raja Casablanca dhidi ya Vipers kutoka Uganda.

Kocha Mkuu wa Simba, Roberto Oliveira 'Robertinho' alisema kikosi chake kiko tayari kuwavaa Horoya na ana matumaini ya kufanya vyema katika mchezo huo ili kujiweka katika nafasi nzuri ya kusonga mbele kwenye michuano hiyo.

Robertinho alisema anafahamu ugumu wa mechi hiyo lakini pia kumkosa kiungo mshambuliaji wake, Saidi Ntibazonkiza anaamini ana wachezaji wengine wazuri ambao wataweza kupambana kusaka matokeo mazuri.

Kocha huyo alisema Simba itafanya vizuri katika mechi hiyo na kuongeza kikosi chake kina wachezaji wazoefu wanaoijua vyema michuano hiyo.

"Mechi zote tutakazocheza ni ngumu na zitakuwa na ushindani, kwa sababu tunaanzia ugenini, tutapambana kuhakikisha tunapata ushindi na kurejea nyumbani tukiwa na nguvu ya kuendelea kupambana, tukipata matokeo mazuri, yatatuwekea wepesi kuelekea mchezo unaofuata ambao tutakuwa nyumbani," alisema Robertinho.

Mratibu wa Simba, Abbas Ally, alisema maandalizi yote muhimu kuelekea mechi hiyo yamekamilika na mpaka sasa hakuna kitu chochote ambacho si cha kawaida kilichowatokea.

Abbas alisema kila mchezaji anafahamu kazi iliyowapeleka huko na wamejipanga kuonyesha kiwango bora ili wafikie malengo ya timu.

"Hakuna chochote kibaya au hujuma kwa sababu moja ya kazi ya mimi kufika huku mapema kabisa ni kuangalia, kuzuia na kuzima njia zote ambazo zinaweza kufanya timu isiwe kwenye hali ya utulivu na akili ielekezwe katika mechi tu.

Hali ya hewa ya Guinea haitofautiani na ya Dar es Salaam kwa kipindi hiki, tangu mimi (Abbas), nimekuja hapa nina siku ya sita, nyuzi joto ni zile zile tu kuanzia 30 au 28, ukiangalia na huko kabla ya hizo mvua za huko hazijanyesha hali ya jotoridi ni lile lile, na hata hali ya hewa pia zinafanana kwani mji wa Conakry nao uko baharini kama Dar tu," alisema Abbas.

Hata hivyo alisema mashabiki wa soka wa Conakry wametabiri mechi hiyo itakuwa ngumu kwa sababu wanaitazama Simba kama moja ya timu kubwa barani Afrika.

"Mashabiki wa hapa wanaizungumzia mechi hii itakuwa ngumu, wao wanajua timu yao inakwenda kukutana na timu ngumu, timu bora kwenye viwango vya CAF, lakini cha msingi na kukumbuka mechi hii Horoya hawatocheza na mashabiki kwa sababu uwanja wao umefungiwa, wameruhusiwa kucheza hii mechi, michezo mingine miwili hawatacheza nyumbani, watakwenda Senegal au Mali," alisema kiongozi huyo.

Horoya tangu Januari 21 haijacheza mechi yoyote ile ya ligi baada ya Chama cha Soka cha Guinea kusimamisha mechi zao kwa ajili ya kuipa nafasi kujiandaa kukabili Simba.

Wakati huo huo, Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, amezitakia kila la heri timu za Simba na Yanga ambazo zinakabiliwa na majukumu ya kimataifa huko ugenini.

Majaliwa alisema hayo jana alipokuwa akilifunga Bunge la Jamhuri ya Muungano, jijini, Dodoma.

INAENDELEA UK 23


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >